**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**
**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani. |
| 9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |
| 12.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando |
| 13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa. |

| | |
|---|---|
| 14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi |
| 18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Othman Masoud Othman | Mwanasheria Mkuu |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae |

| | |
|---|---|
| 30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 32.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 33.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 34.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 35.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 37. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 38.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 40.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 44.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 45.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 46.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 47.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 51.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |

| | |
|---|---|
| 53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | Jimbo la Kiembesamaki |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kateuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 59.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 65.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 66.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 67.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 70.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 71.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 72.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 77.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Pili – Tarehe 17 Januari, 2013**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa heshima na ruhusa yako, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya 2006, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Hassan Hamad Omar (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya 2006, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 112**

**Matumizi Mabaya ya Fedha za *SACCOS* Kinyume na Taratibu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Alijibu:-

Kuna *SACCOS* inaitwa *WARIDI* iliyopo Chwaka ambayo imetumia fedha kinyume na utaratibu. Wizara iliweka ahadi kufuatilia marejesho ya fedha hizo zilizotumika kinyume na utaratibu.

(a) Je, wizara inasema nini juu ya ahadi hiyo.

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 112 kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli ipo "*WARIDI SACCOS*" ambayo imesajiliwa rasmi na serikali kupitia Idara ya Ushirika Zanzíbar na kupewa Hati ya Usajili yenye nambari 2687/2005. *SACCOS* hiyo ina vituo vitano vifuatavyo:-

- Kiembesamaki,
- Fuoni,
- Mkokotoni,
- Chwaka na
- Matemwe.

Mhe. Spika, Makao Makuu yake yalikuwa Wilaya ya Mjini eneo la Posta Kijangwani, *WARIDI SACCOS* ilikuwa ikitoa huduma za kifedha kwa wanachama wake kwa kupitia vituo vyake ambavyo hufuata taratibu zote za uwekaji akiba na utoaji wa mikopo, pia hudhaminiana kupitia vikundi na vituo vyao.

Kituo cha Chwaka **"**TWENDE SALAMA" kilichukua mkopo kwa mujibu wa sera ya mikopo ya *"WARIDI SACCOS"* kwa lengo la kukuza mitaji yao na kuendeleza biashara zao, ambazo walitakiwa kurejesha mikopo kwa mujibu wa sera na taratibu zilizopangwa. Kwa bahati mbaya, sehemu ya mikopo hiyo haikurejeshwa ipasavyo. Aidha sababu kubwa iliyotolewa na wanachama ni kuzorota kwa biashara zilizoombewa mikopo hiyo.

Kwa hivyo bado wanachama tisa hawajakamilisha marejesho ya mikopo yao yenye thamani ya jumla ya shilingi 2, 763,000/=. Wizara yangu kwa mashirikiano na Wizara ya Ustawi wa Jamiii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto imefuatilia na kuchukua hatua mbali mbali kama hizi zifuatazo:-

- Kumefanyika kikao cha pamoja na Uongozi wa Wilaya ya Kati na Maafisa Ushirika, Wanawake na Watoto na Viongozi wa *WARIDI SACCOS* pamoja na baadhi ya wanachama wa Kituo cha Chwaka, ili kujadili tatizo hilo.

- Kumefanyika kikao chengine cha pamoja huko Chwaka ambacho kiliwashirikisha Wanachama wa Kituo cha Chwaka, Afisa Ushirika na Afisa Wanawake na Watoto na Viongozi wa *WARIDI SACCOS*. *Agenda* kuu ni kuweka mkakati wa kuhakikisha kuwa marejesho ya mkopo yanafanywa, kwa kuwahusisha wadhamini wa mikopo.

- Pia kilifanyika kikao cha pamoja baina ya Uongozi wa Idara ya Ushirika na Uongozi wa *WARIDI SACCOS*, lengo ni kutathmini utekelezaji wa ahadi na maagizo yaliyotolewa Ambayo yanataka kuona wakopaji wanarudisha madeni hayo. Hata hivyo kasi ya urudishaji mikopo ni ndogo.

b) Wizara itaendelea na zoezi la ufuatiliaji wa madeni kwa wanachama wa *WARIDI SACCOS* na wengine wote na kuhakikisha kuwa wale wote wanaohusika wanarejesha mikopo hiyo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana.

(a) Kabla ya *SACCOS* hii kupatiwa fedha kuna mafunzo gani yalifanyika kwa wanachama wa *SACCOS* hii, ili mradi uwe endelevu na wahusika waweze kurudisha mikopo hiyo.

(b) Baada ya kutokea matatizo, wizara imefanya utafiti kuangalia sababu zipi za msingi *SACCOS* hii kutofikia malengo.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Spika.

(a) Kwa kawaida kikundi chochote cha ushirika au *SACCOS* yoyote kabla hawajaanza shughuli zao hupita taratibu za kuomba na kusajiliwa na kwenye hatua za mwanzo ni kuhakikisha kuwa tunavipatia mafunzo pamoja na taaluma kuhusiana na vikundi vyao vya *SACCOS* au vyama vya ya ushirika.

(b) Mhe. Spika, naomba kidogo arejee kwa sababu sikulifahamu vizuri.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, rejea swali (b).

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana baada ya kutokea matatizo wizara imefanya utafiti kuangalia sababu zipi za msingi.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika:** Mhe. Spika, utafiti umefanyika kwa kuzipitia *SACCOS* zote pamoja na Vyama vya Ushirika karibu 5000 na tukagundua kwamba Vyama vya Ushirika pamoja na hizi *SACCOS* ambazo ziko hai ni karibu 1604 na tumeanza na tunaendelea kutoa mafunzo na hata hii *WARIDI SACCOS* ilipatiwa mafunzo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, hivi sasa tumetoa mafunzo karibu vikundi kama 464 vimepatiwa mafunzo na tunaendelea na juhudi hizo.

**Nam. 68**

**Kukosekana kwa Huduma ya Chakula katika Hospitali ya Mnazi Mmoja**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) -** Aliuliza:-

Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio hospitali kubwa pekee ya serikali hapa Zanzibar, na kwa kuwa hospitali hiyo ndio kimbilio la watu wenye kipato cha chini kwa maana ya wakwezi na wakulima.

Na kwa kuwa hadi kufikia Oktoba 2012 kuna taarifa kuwa ni karibu miezi 6 hospitalini hapo, hapapikwi chakula cha wagonjwa, na hivyo kukosekana kabisa kwa huduma hiyo jambo ambalo linaleta usumbufu mkubwa kwa walengwa (wakwezi na wakulima).

(a) Je, serikali inalifahamu suala hilo.

(b) Ni sababu gani ya msingi iliyopelekea huduma hiyo isitolewe.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Serikali inalifahamu hilo.

(b) Sababu za msingi zilizopelekea huduma hiyo isitolewe ni kama ifuatavyo:-
Hospitali ya Mnazi mmoja ina sehemu tatu kuu, nazo ni Mnazi Mmoja yenyewe, Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu na Hospitali ya Wazazi Muembeladu ambazo zinatakiwa kupewa huduma ya chakula.
Ili hospiali hizo tatu ziweze kupatiwa chakula panahitajika kwa mwezi shilingi milioni 6.6. Pesa za chakula zinatoka kwenye mgao wa serikali katika matumizi mengineyo "*OC*", na hilo linategemea serikali imekusanya mapato kiasi gani kwa mwezi ule na Wizara ya Afya inapewa fungu lake kwa matumizi ya Wizara ikiwemo hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa kawaida wizara ikishapata *OC* inakaa na idara zake zote na wanagawana kilichopatikana kwa mujibu wa vipaumbele na unyeti wa masuala yaliyojitokeza wakati wa mgao. Idara ya Mnazi Mmoja huwa ni ya pili kwa umuhimu baada ya mgao wa Mfamasia kwa ajili ya dawa.

Mnazi Mmoja wakishapewa fungu lao nao wanagawa mafungu yao kwa mujibu wa kilichopatikana na kwa vipaumbele vyao.

Vipaumbele vya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambavyo muhimu ni *Oxygen*, *Diesel* kwa ajili ya genereta la dharura na gari ya kuchukulia madaktari wa dharura wakihitajika, vifaa vya usafi na kwa chakula kwa Hospitali ya Kidongo Chekundu, posho za madaktari, na baadaye mengineyo mengi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Kila mwaka Baraza lako tukufu linaidhinisha fungu la fedha za chakula kwa sababu gani isipatikane huduma hiyo ya msingi kwa wananchi hao.

(b) Ni kampuni gani ambayo ina zabuni na kutoa huduma ya chakula Hospitali ya Mnazi Mmoja, Kidongo Chekundu na Mwembeladu.

(c) Kuna taarifa Hospitali ya Kidongo Chekundu ya Wagonjwa wa Akili wanakula mlo mmoja tu na dawa wanazozitumia ni nzito haikidhi. Je, serikali inalitambua suala hilo na itachukua hatua gani kwa wanyonge hao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, tunafahamu kwamba chakula ni muhimu na kama tungekuwa tunao uwezo basi tungekuwa tunawapa wagonjwa chakula, na kweli mafungu yanapitishwa hapa na sote tunafahamu, lakini tunachopewa si lazima kiwe kilichopitishwa.

Kwa hiyo, kile tunachokipata ndicho tunachokitumia na kwa kutizama umuhimu wa wagonjwa wanaopewa chakula, basi ndio maana Kidongo Chekundu imepewa umuhimu kwa sababu wale ni wagonjwa wa kipindi kirefu na ndugu zao wanachoka kuwapelekea chakula kama alivyosema Mhe. Mjumbe kwamba dawa wanazokula ni kali, lakini bado tunachokipata ndicho tunachokitumia.

Kwa kweli, ndio maana vipaumbele vya Idara ya Hospitali ya Mnazi Mmoja imeipa umuhimu Kidongo Chekungu Hospital kwa ajili ya chakula na hata kama ni mlo mmoja huo ndio tulioumudu.

**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri, swali (b) kampuni iliyopewa zabuni.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, hakuna kampuni yenye zabuni, isipokuwa chakula kinanunuliwa na serikali na Uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio unaofanya kazi hiyo na wala hatuna zabuni kwa ajili ya chakula cha hospitali.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, rudia swali (c).

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante sana kuna taarifa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu wanapata mlo mmoja tu kwa siku, je serikali inatambua hilo na hatua gani zitachukuliwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nafikiri nimelijibu kwenye majibu yangu ya mwanzo kwamba Hospitali ya Kidongo Chekundu ndio hospitali pekee inayopatiwa chakula na tunachokipata baada ya kuwagawia hicho tunachokipata na wale wanao watu wao, lakini kama tunapata mlo mmoja basi tunawapa mlo mmoja na tutatoa milo mitatu wakati hatuna fedha na ndugu zao wanawaletea, isipokuwa sisi tunajitahidi.

Kwa upande wa Hospitali ya Mnazi mmoja na Mwembeladu itakosa lakini tunajitahidi angalau huo mlo mmoja upatikane huko Kidongo Chekundu, na kama umesikia ni kweli na inapopatikana mitatu wanapewa mitatu.

**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Hivi ni kiasi gani kwa siku mgonjwa aliyelazwa anahitaji kupatiwa kwa ajili ya chakula cha kutosha ukizingatia mahitaji na maradhi mbali mbali na bajeti mliyonayo ya chakula kwa kila mgonjwa kwa sasa ni kiasi gani. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, tukiangalia mgonjwa mmoja mmoja na matatizo waliyonayo, kwa kweli wagonjwa wetu wanatafautiana. Kwa mfano, wagonjwa wa *pressure* wanakula tafauti, wasukari wanakula tafauti na kama tunataka kuwa wakweli hasa kwa ajili ya

kuwapatia chakula, basi kwa siku angalau mgonjwa mmoja kama huyu anatakiwa shilingi 10,000/- ili kukidhi haja.

Lakini tukitizama mgao wetu hivi sasa kwa hospitali zote hizo kila mgonjwa anapata shilingi 500/-, kwa hiyo 500 tukizikusanya pamoja tunapeleka Hospitali ya Wagonjwa wa Akili na wala Hospitali ya Mnazi mmoja na hata Mwembeladu hatuwapi.

**Mhe. Salmin Awadh Salmin:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Wakati Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba mahitaji ya chakula kwa mwezi katika hospitali hizo alizozitaja ni shilingi milioni 6 kwa mwezi.

Je, Mhe. Waziri hivi sasa anapata kiasi gani kwa mwezi kwa ajili ya chakula cha wagonjwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwa mwezi huwa zinatafautiana na sio kila mwezi tunapata mgao ule ule, kwa kweli mgao tunaoupata siku zote kwa miezi hii mitatu uko chini angalau kwa miezi mitatu ambayo ninaifahamu uko chini.

Kwa hivyo, tukishapata sasa tunapata fungu la Hospitali ya Mnazi mmoja na tunapopewa fungu la Hospitali ya Mnazi mmoja na hapo hatusemi kwamba hizi ni fedha za chakula, isipokuwa tunaweka vipaumbele kama hivyo nilivyovitaja kama vile *diesel, oxygen, generator*, maji, kuchukulia wagonjwa na hivyo ndivyo vipaumbele vya mwanzo na chakula kinafuata huko chini, na chakula ambacho tunakiweka hasa ni Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu basi.

Kwa mfano, kwa mwezi huu fedha tulizopata nafikiri shilingi 10,000/- kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na tukitoa 6.6 tukawapa chakula hayo mengine tutayafanyaje.

Kwa hivyo, siku zote mgao wetu wa Hospitali ya Mnazi mmoja haututoshi na tukiweka vipaumbele chakula kwa kwetu kinakuwa sio kipaumbele kusema kweli, kwa sababu kipaumbele kwa masikini au mgonjwa na tunafahamu hilo, lakini kama madaktari dawa, *oxygen*, daktari wa dharura pamoja na posho ya daktari hivyo kwetu ndio kipaumbele.
**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri, umetaja shilingi 10,000/- hebu iweke sawa hiyo, yaani umetaja kwa mwezi huu mumepata shilingi 10,000/- hivi ni sawa au sikusikia vizuri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwa Hospitali ya Mnazi mmoja ni shilingi milioni 10.

**Nam. 111**

**Mchakato wa Kuanzisha Mabaraza ya Watoto Vijijini**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:-

Katika kikao cha Bajeti cha mwaka 2012/13 Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, ilitoa ahadi ya kuandaa utaratibu wa kuunda au kuanzisha Mabaraza ya Watoto Vijijini.

Je, suala hili limefikia wapi.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto -** Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa katika kikao hichi muhimu kwa mwaka huu wa 2013. Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 111 kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto katika Kikao cha Bajeti ilitoa ahadi ya kuunda Mabaraza ya Watoto katika Shehia na Wilaya za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ninapenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba, hatua hiyo ya kuunda Mabaraza tayari imeanza kufanyiwa kazi. Kwa kweli mpaka hivi sasa tayari tumeshaweza kuunda Mabaraza 108 ya Watoto yameshaundwa katika Wilaya za Pemba na Mabaraza 87 kwa Wilaya za Unguja na bado mchakato unaendelea.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri.

(a) Hivi imekuwaje kwanza kuunda Mabaraza ya Vijana kabla ya kuunda Mabaraza ya Vijana wa Taifa ambapo msingi wake ni Baraza la Vijana wa Wilaya.

(b) Kuchelewa kuunda kwa Baraza la Vijana la Taifa na kujadili mambo yao ikiwemo tatizo la dawa za kulevya pamoja na tatizo la maradhi ya UKIMWI.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, swali liliopo mbele yangu ni suala la kuunda Mabaraza ya Watoto sasa kuchelewa kuundwa kwa Baraza la Vijana pamoja na mabaraza mengine ya taifa Mhe. Spika, naona hili halihusiani na Mabaraza ya Watoto.

## UTARATIBU

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, jirani yangu hapa Mhe. Ismail Jussa Ladhu jana alizungumza na kama kukataa unaweza kuangalia wewe Mhe. Spika, lakini ukilitizama hili swali halitaki hata tochi kumurika linahusu swali la msingi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, sijafahamu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, Mhe. Waziri hawezi kukataa swali, isipokuwa mwenye haki ya kukataa kwa hapa kwa mujibu wa kanuni ni wewe Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mjumbe, alichosema Mhe. Waziri ni kwamba Mabaraza ya Watoto na Mabaraza ya Vijana ni vitu viwili tafauti ndicho alichosema. Sasa kama hivyo ndivyo basi wewe sasa uulize swali linalohusu Mabaraza ya Vijana.

Kwa kweli hicho ndicho alichokisema Mhe. Waziri, sasa kuwa ndivyo au sivyo hiyo nadhani mawaziri wenyewe wapo wanaweza kusawazisha, lakini alichokieleza ni kwamba Mabaraza ya Watoto na Mabaraza ya Vijana ni vitu viwili tafauti.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa msaada wako. Sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba wizara yake imeunda Mabaraza ya Watoto kwa Unguja na Pemba katika kila shehia na mabaraza haya yamo kwenye majimbo ya Unguja na Pemba.

Vile vile Kamati yetu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilizungumza na wizara yake na kukubaliana kwamba kila jimbo Mabaraza ya Watoto haya wakabidhiwe Wawakilishi na Wabunge, ili wawe karibu na watoto wao.

Kwa hivyo, ni sababu zipi ambazo hadi leo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hawajakabidhiwa mabaraza hayo, ili tukayajua mabaraza hayo kwa Unguja na Pemba, kwa ajili ya kuwasaidia na kuwaelekeza.

**Mhe.Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, nashukuru kwa swali la Mhe. Mjumbe. Lakini tulivyokubaliana ni kwamba tutaunda Mabaraza ya Watoto kupitia shehia, wilaya pamoja na mikoa yao, sasa haya mambo ya jimbo na mengine naomba radhi kidogo sijui kama nimelifahamu hili swali.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa kuwa kwenye swali lake mama Mhe. Waziri alisema katika Wilaya za Pemba ni Mabaraza 108 yaliyoundwa na Unguja 87 kama nimesikia vizuri. Naomba nimuulize Mhe. Waziri kati ya mabaraza hayo kwa wilaya ya Pemba yameundwa mabaraza mangapi kwa kila wilaya.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, ahsante kwa bahati nzuri mabaraza yote ambayo tayari yameshaundwa ninayo hapa, yaani kila wilaya pamoja na shehia mabaraza yapo na ninayo hapa. Kwa mfano, Mkoani, Kangani yapo, yaani kila ilipokuwa baraza limeshaundwa basi tayari na orodha hii hapa ninayo na mimi mwenyewe nimehakikisha kwamba kweli yameshaundwa kwa kuyapitia mabaraza moja baada ya moja.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, alichokuwa anahitaji Mhe. Mjumbe ni kujua kila wilaya ni mabaraza mangapi. Kwa hiyo, kama unayo hapo basi mtajie tu.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, wilaya zinatafautiana. Kwa mfano, Wilaya ya Kusini Unguja kuna mabaraza kumi (10).

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, Mhe. Mjumbe ametaka kwa upande wa Pemba tu.

**Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, mabaraza ya Wilaya ya Wete Pemba yapo 13, Wilaya ya Micheweni 11, Wilaya ya Chake Chake 29 na Wilaya ya Mkoani 13. *(Makofi)*

**Nam. 117**

**Kupatiwa Boti Wananchi wa Jimbo la Muyuni**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub -** Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu, kwanza naomba uniruhusu nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwake na hii inatokana na umakini wake wa hapa Barazani pamoja na wananchi wake. Baada ya maelezo hayo naomba sasa swali langu Nam. 117 linalohusu wananchi wa Jimbo la Muyuni na mimi kama ni mtumishi wao waliyeniajiri na tulikuwa watu 11 na wakaniamini mimi kuja kutetea haki hii. *(Kicheko/Makofi)*

Katika Mkutano wa Bajeti uliopita serikali iliahidi kuwapatia wananchi wa Jimbo la Muyuni boti kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

(a) Kwa nini hadi hii leo ahadi hiyo haijatekelezwa.

(b) Mhe. Waziri huoni kuwa kutoa ahadi hiyo mbele ya chombo hichi muhimu kwa wananchi na kutoitekeleza ni kuwavunja moyo wananchi hao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kabla ya kujibu swali la Mhe. Mjumbe Nam. 117, kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi kwa ufuatiliaji bora wa mambo yanayohusu wananchi wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 117 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ahadi ya kuwapatia wananchi wa Jimbo la Muyuni boti kwa ajili ya uvuvi tayari imekwishakamilika.

Boti ilikabidhiwa awali lakini kulitokea mzozo kati ya wavuvi wenyewe kwa wenyewe juu ya matumizi ya boti hiyo na wizara ikalazimika kuichukua na kuihifadhi boti hiyo, ili kuweza kupata suluhu. Aidha baada ya makubaliano kupatikana, wizara imerejesha boti hiyo kwa wavuvi wa Jimbo la Muyuni.

b) Mhe. Spika, kwa vile ahadi hiyo imekwishatekelezwa na wizara, basi naamini jamii kubwa ya wavuvi wa Muyuni tayari wamekuwa na imani na serikali pamoja na Wizara yao ya Mifugo na Uvuvi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, ahsante, lakini nataka kumwambia Mhe. Naibu Waziri kwamba la Muyuni nalijua mimi na la Mpendae atakuwa analijua yeye. Kwa hivyo, baada ya kikao hichi kwa gharama zangu na wala sina nia kama nataka kuonesha jeuri kwenye Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika, nitagharamia mafuta pamoja na Wajumbe wake akanioneshe hiyo boti iko pahala gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika, Wizara yangu iko tayari kufuatana na yeye iende kumuonesha hizo boti zilizokabidhiwa na siku iliyokabidhiwa. Vile vile wizara yangu itatumia usafiri wake ili hiyo gharama aliyosema ichangie wizara yangu apeleke kwa wananchi wake ili iwasaidie. (*Makofi*)

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nimuulize kwa ufupi kama ifuatavyo.

Kwa kuwa amekiri kwamba boti imenunuliwa ingawa kulikuwa na mgogoro kati ya washirika wa boti hiyo. Ni sababu zipi za msingi ambapo muda wote huo wizara imeshindwa kutatua mgogoro huo na leo mwakilishi anahoji suala hilo la boti. Naomba anieleze ni sababu zipi za msingi na ni nani aliyesababisha sababu hizo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi:** Mhe. Spika**,** wizara yangu haijashindwa kutatua mgogoro wowote unaotokana na uvuvi na jitihada kubwa zinachukuliwa na Idara yangu ya Maendeleo ya Uvuvi kutatua migogoro yote na ndio maana baada ya kutatua migogoro hiyo tukawakabidhi wananchi wale boti yao na sasa mambo yanakwenda sawa kabisa.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya Mwaka 2006

*(Kusomwa kwa mara ya pili)*

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Uchukuzi:** Mhe. Spika, nakushukuru kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai uzima na taufiqi wa kufika hapa. Pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuhudhurisha mbele ya Baraza lako tukufu marekebisho ya Mswada wa Sheria Nam. 5 ya mwaka 2006 ya Mamlaka ya Usafiri Baharini ZMA.

Mhe. Spika, kabla sijahudhurisha marekebisho au muhtasari wa marekebisho hayo naomba nitoe taarifa fupi kwa ruhusa yako. Katika kipindi ambacho nilikuwa Mwakilishi Miswada ya

marekebisho mengi ilikuwa tukipata tabu iwapo marekebisho hayakuwekwa wazi wazi kwa kufanyiwa ufafanuzi. Kwa hivyo nimetoa karatasi yenye kurusa saba ambayo tumewagaiya wajumbe wote ambayo inabainisha pale marekebisho yatakavyofanywa na sasa kifungu hicho kitasomeka vipi. Kwahivyo itakuwa ni rahisi kwa wajumbe nadhani kusoma marekebisho kamili kwamba baada ya marekebisho kifungu kitasomeka kama kinavyoonekana katika karatasi ambazo tumegawa.

Baada ya taarifa hiyo Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa nihudhurishe muhtasari wa Mswada wa Marekebisho ya Sheria Nam 5 ya Mwaka 2006 ya Mamlaka ya Usafiri Baharini yaani *Zanzibar Maritime Authority.*

Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri Baharini ni taasisi iliyosimama kwa Sheria Nam. 5 ya Mwaka 2006. Taasisi hii inasimamia usajili wa meli za ndani na pia tuna usajili wa meli za kigeni ikisaidiwa na wakala huko Dubai.

Mhe. Spika, taasisi hii pia inasimamia uendeshaji wa shughuli za usafiri ikiwa ni pamoja na uzima na ubora wa vyombo vya baharini na hali ya usalama wa abiria na mabaharia ndani ya vyombo hivi vinavyosafiri.

Mhe. Spika, baada ya kutokezea ajali ya MV. Spice Islanders mwaka 2011, serikali iliunda Tume na kutoa mapendekezo mbali mbali kwa baharti mbaya sana Zanzibar ilipata tena mshtuko kwa kutokezea ajali ya pili mwaka 2012 ikiwa ni chini ya mwaka mmoja tokea ajali ya MV Spice Islanders.

Mhe. Spika, hali hii ya mtafaruku ilipelekea kujichukunguza upya mapungufu tuliyonayo katika usimamizi wa usafiri wa baharini na aina ya vyombo vinavyotumika. Ilikuwa ni jambo la wazi kuwa mabadiliko yanahitajika katika kuchunga usalama wa watu wetu na wageni wanaposafiri.

Mhe. Spika, Mswada huu unakusudia kufanya marekebisho na kuleta mabadiliko katika:

1) Uendeleshaji wa majukumu ya taasisi hii ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini.

2) Kuchunguza na kutilia mkazo zaidi juu ya usalama wa abiria na mabaharia katika vyombo vyetu.

3) Kuweka msisitizo juu ya matumizi ya vyombo vyenye ubora na viwango ulikilinganisha na sheria za kimataifa za *International Maritime Organization (IMO*)

4) Kuendeleza ukaguzi wa kina na wa kila kipindi kwa kawaida na wa ghafla pale itakapotokea haja.

5) Kupata wawekezaji waliomahiri na wenye uwezo wa kukabiliana na hali inayojitokeza zinavyotokea ajali au uwezo wa kujikinga.

Mhe. Spika, kwa nia njema kabisa na kwa kuangalia maslahi ya wananchi wetu kiusalama na kiustawi nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili Mswada huu na kutupa mapendekezo yenye muelekeo wa kuelekea pazuri zaidi na baadae waupitishe.

Mhe. Spika, naomba ku toa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Hassan Hamad Omar (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Mawasiliano na Ujenzi naomba kusoma hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam.5 ya Mwaka 2006.

Mhe. Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana asubuhi hii ya leo na kujadili Mswada huu muhimu wa kuirekebisha Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya Mwaka 2006.

Mhe. Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusiana na Mswaada huu tunaoujadili. Baada ya kutoa shukurani, nitangulie kusema kuwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inaunga mkono uamuzi wa Serikali wa kuleta Mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuiboresha sekta ya usafiri wa Baharini ambayo imekua na changamoto nyingi hivi sasa ambapo kwa namna moja ama nyengine marekebisho haya yatasaidia kuzitatua baadhi ya kero na changamoto hizo.

Mhe. Spika, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ilipitia Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 ya mwaka 2006. Naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati hiyo walioshiriki kwa ukamilifu katika kazi hiyo kama ifuatavyo:

1. Mhe Makame Mshima Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
4. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
5. Mhe. Subeti Khamis Faki - Mjumbe
6. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Waziri Kheir - Katibu
8. Ndg. Maryam Rashid Ali - Katibu

Mhe. Spika, sasa naomba uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ya Kamati yaliyofanywa na Kamati yetu baada ya kuupitia Mswada huu kama ulivyotuelekeza.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2012, Kanuni ya 83 (5) na (6) ambapo Kanuni hizo zinatoa fursa ya kuwaalika wadau wa sekta husika katika

kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada husika. Kamati ilifanya hivyo kama Kanuni inavyoelekeza ambapo wadau wa sekta ya Usafiri wa Baharini walifika na kutoa maoni yao kuhusiana na Mswada huu. Kwa msingi huo, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa wadau wote walioshiriki kutoa maoni yao ambayo yameisaidia sana Kamati katika kufanya marekebisho haya, mawazo ya wadau hao yanaheshimwa sana na tunapenda kuchukua nafasi hii kuwaeleza wadau wote kuwa wasichoke kutusaidia pale tunapohitaji msaada wao.

Mhe. Spika, kutokana na kukua kwa sekta ya utalii na sekta ya usafiri kwa ujumla, ni wazi kuwa kuna haja kubwa ya kuzirekebisha sheria zetu na kuzifanya ziwe bora zaidi ambapo zitasaidia kuwaongoza wadau wa sekta hiyo na kurahisisha usafiri wa baharini kwa wananchi walio wengi.

Aidha kuimarika kwa sekta ya usafiri wa baharini kutaongeza ari ya ushindani wa kibiashara miongoni mwa wafanyabiashara na kuimarika sekta ya utalii ambayo inasaidia pato la taifa kwa kiasi kikubwa na kuitangaza nchi yetu Kimataifa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Mswada huu, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini hivi sasa imepewa uhuru wa kushirikiana na taasisi nyengine hapa nchini kwa lengo la kusimamia ipasavyo sekta ya usafiri ili kuepusha maafa ambayo yamekuwa yakilikumba taifa letu hivi karibuni na kusababisha vifo vya wananchi wasiokua na hatia. Aidha ushirikiano huu tunaamini utaleta faida kwa pande zote zitakazoshiriki na kusaidia kurudisha imani ya wananchi kwa Serikali yao.

Mhe. Spika, Katika kifungu cha (6) cha Mswada huu kinachohusu ushirikishwaji wa SUMATRA katika usimamizi wa mambo ya Usafiri wa Baharini, Kamati imependekeza kuwa neno "SUMATRA" lisiwekwe moja kwa moja na badala yake liwekwe neno "Mamlaka" inayosimamia mambo ya Usafiri wa Baharini Tanzania.

Mhe. Spika Kamati imependekeza kuwekwa kwa neno hilo ili kuepusha kujifunga kwa Mamlaka kwa taasisi hiyo kutokana na historia yake iliyopita huko nyuma ambapo kulikuwa na kutokuelewana kusikokuwa kwa lazima, hivyo Kamati imeona ni busara kuweka neno hilo ili kuiweka Mamlaka katika nafasi yake inayostahiki.

Mhe. Spika, Kamati yetu pia inapendekeza kurekebishwa kwa kifungu cha 99 cha Mswada huu kinachotaka kuondoa neno "wafanyakazi" na kuweka neno "mabaharia" ambapo Kamati imependekeza katika kifungu hicho neno "wafanyakazi" lisiondoke na badala yake liongezwe na neno "mabaharia" ili kuwatofautisha watu hao na kila mmoja aweze kuwajibika kisheria na kuujua wajibu wake katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Mhe. Spika, kamati pia ilipokea na kuyakubali baadhi ya marekebisho kutoka Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambapo marekebisho hayo yamepokelewa kutokana na kuzingatiwa mambo ya Msingi yakiwemo yaliyoainishwa katika ripoti za matukio ya kuzama kwa meli. Aidha marekebisho hayo yanajumuisha vifungu vifuatavyo:

Kifungu cha 7 (8) ambapo kifungu hiki kinaruhusu Mkurugenzi wa Mamlaka pia kuwa Mrajisi wa Meil ambapo pia Mkurugenzi huyo huyo kuwa Mrajisi wa Mabaharia. Hivyo kama ilivyo

katika ripoti ya tume ya ajali ya M.V Skagit ambayo ilipendekeza kifungu hicho kifutwe, wizara imeliona hilo na imeleta marekebisho hayo ya kukifuta kifungu hicho na Kamati imeridhia.
Kifungu cha 207 (2) ambapo kifungu hiki kama ilivyopendekezwa na tume kumpa uwezo Mrajisi wa kudai cheti cha usajili kimerekebishwa na uwezo huo hivi sasa umewekwa wazi kama ilivyopendekezwa.

Kifungu cha 12 kimeongezwa kifungu kipya cha (3), kifungu hiki kimeweka wazi mitaji ambayo meli zinalazimika kuwa nayo. Kama ilivyopendekezwa na Tume kifungu hiki kimezingatiwa na Kamati imeridhia kuwepo kwa kifungu hiki.

Kifungu cha 122(a) kimeongezewa kifungu kipya cha 122(a) (1) ambapo kifungu hicho kinaelezea umuhimu wa kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi na uwezo katika uendeshaji wa shughuli zilizomo katika meli. Kutokana na umuhimu wa jambo hilo, Kamati imekiridhia kifungu hicho.

Kifungu cha 57 (2) kimeongezwa kifungu kipya cha 57 (2) (a) ambapo kifungu hiki kinazitaka kampuni za meli kuhakikisha kuwa zinaweka bima kwa ajili ya abiria watakaoathirika endapo ikitokea ajali. Aidha kifungu hicho kimeweka wazi kiasi cha fedha ambacho abiria anapaswa kulipwa endapo ikitokea ajali. Kamati imeyapokea na kuyakubali marekebisho hayo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa tunaiomba serikali kuyazingatia yale yote yanayopendekezwa na tume, kamati au wadau wa taasisi husika pindi wanapotoa mapendekezo kuhusiana na jambo husika. Kufanya hivyo ni kuisaidia serikali na taasisi husika kuepukana na majanga ambayo baadhi ya wakati yanaweza kuepukika. Aidha Kamati inapenda kuishauri Mamlaka ya Usafiri Bharini kufanyakazi kwa ushirikiano na sekta binafsi ili kuiimarisha Mamlaka hiyo ambayo inahitaji kuimarishwa kwa kiwango cha hali ya juu.

Mhe. Spika, endapo marekebisho ya Sheria hii yatapita, Kamati yetu inaamini kuwa kutakuwa na sheria bora zaidi kwa madhumuni ya kuratibu shughuli za usafiri baharini. Hata hivyo, Kamati yetu inasisitiza umuhimu wa kutekeleza sheria hii kwa umakini mkubwa ili kunusuru majanga yasiyo ya lazima.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo, tunawaomba Wajumbe wenzetu wauchangie Mswada huu kwa kutoa mawazo yatakayosaidia katika kuufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

## UTARATIBU

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Spika, naomba kuhusu utaratibu nataka niitumie Kanuni ya 84 katika kutoa muongozo wako.
Mhe. Spika, kifungu cha 84 cha Kanuni yetu kimeelezea namna Mswada utasomwa kwa mara ya pili na kuwasilishwa mbele ya Baraza letu. Katika hilo nakumbuka tulitoa maagizo Waheshimiwa Wajumbe kwamba, Miswada inayohusiana na marekebisho ya sheria ni lazima

Mawaziri watuletee Sheria Mama ili tupate kufanya *reference* kwa sababu Wajumbe waliowengi katika kipindi hicho walikuwa hawapo na kuwaletea marekebisho tu pasi na kuwaletea Sheria Mama kwa kweli inakuwa hatuifanyii haki Miswada hiyo. Hivyo ni sawa na Wawakilishi kufanya kitu ambachokuwa hatukijui. Kitu hicho ni hatari sana kwa uhai wa taifa letu.

Mhe. Spika, naomba niombe muongozi wako kwamba tuwatake Mawaziri, tuakhirishe kwa muda ili Mawaziri watupatie Wajumbe nakala za Sheria Mama ili baadae tuendelee na mjadala huu. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Nakala za Sheria Mama zinahitajika ili Wajumbe wawe wanafuatilia marekebisho. Kwa maana hiyo mjumbe anaomba tuakhirishe ili tuweze kufanya hivyo.

Ninachokikumbuka Mhe. Waziri alichosema inategemea na ukubwa wa sheria yenyewe. Sheria nyengine ni *volume* kubwa kuja kutengeneza kitu cha aina hiyo kwa wajumbe wote kunamatatizo yake kidogo.

Lakini Waziri ametengeneza kitu ambacho sijui kama kimewafika Waheshimiwa Wajumbe? Alisema kwamba hicho ametengeneza maalum kusaidia Waheshimiwa Wajumbe kuweza kufanya rejea na namna sasa kifungu kitakachosomeka. Sijui kama nikosawa alisema hivyo? Wajumbe sijui mmeipata hiyo, ina kurasa saba. Mimi nadhani itoshe ili tuweze kufatilia kwa makini hichi kilichoelezwa.

Madhumuni ndio hayo hayo Mheshimiwa Mjumbe ambayo umetaka tuakhirishe ili kurahisisha kazi hii, Waziri amekwisha kuandaa kitu hichi sina hakika kama unacho laa. Mimi nafikiri tuendelee, sasa Mhe. Omar Ali Shehe kama upo tayari kuchangia uchangie au laa tuone waheshimiwa wengine kama wapo tayari kufanya hivyo.

**Mhe. Asha Bakar Makame:** Mhe. Spika, kwa sababu Mswada huu ni Mswada muhimu sana tena sana. Nafikiri ilikuja mijadala mbali mbali hapa huko nyuma. Lakini nimuunge mkono Mheshimiwa. Kwa kweli ni vyema tukapatiwa Mswada uliopita ili kulipitia suala hili kwa kina Mhe. Spika. Na hayo tuliyoyazungumza na hii karatasi ambayo ametwambia Mhe. Waziri tumeipata hivi asubuhi sasa hivi.

Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, kwa sababu tunajadili Mswada ambao utaleta matumaini kwa wananchi wetu kuhusu suala la usafiri ni suala nyeti Mheshimiwa. Naomba kumuunga mkono Mheshimiwa aliyekaa sasa hivi. Na si Mswada huu tu, miswada yote ambayo inataka kufanyiwa marekebisho ni vyema tukapatiwa Mswada Mama. Amesema Mheshimiwa miongoni walikuwemo, miongoni ni wapya hawajui nyuma kumepitishwa nini. Tafadhali Mhe. Spika. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Spika, Baraza lako litakumbuka kwamba tulirekebisha kanuni na tukasema kwamba Miswada sasa isomwe kwa aina yake. Kwanza unauweka mezani halafu kikao kinachofuata unajadiliwa. Lengo kubwa ni kuwapatia Waheshimiwa Wawakilishi nafasi ya kuupitia huo Mswada. Mswada huu unawekwa mezani katika Kikao kilichopita kwa lengo la kumwambia kila mjumbe kwamba ana haki sasa ya kwenda kuusoma na kuupitia.

Kwenye Library yetu ya Baraza la Wawakilishi sheria hii ipo. Nakumbuka Mhe. Spika, kwamba tulisema nyuma kwa ile Miswada au kwa ile sheria ambazo ni kubwa sana ikiwemo hii. Kwa sababu hii Mhe. Spika, ina vifungu karibu 486. Kwa hiyo haiwezekani kwa sheria yote kwa kila mjumbe kuipata. Sasa tukasema angalau kwa vile vifungu vinavyofanyiwa kazi au vinavyorekebishwa basi vile Waziri anayehusika atakuja na marekebisho yake pamoja na kuvielezea vile vifungu kama alivyosema Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu.

Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wawakilishi kwamba lengo la kuwekwa Sheria Mezani na kusomwa katika kipindi cha pili ni kuwataka wawakilishi wafanye *research* na wasome ile sheria yenyewe na sheria hiyo ipo katika Baraza lako tukufu. Kama pale ambapo Mheshimiwa hakuweza kuifahamu pale ana haki ya kumuuliza katibu, kuwauliza wafanyakazi katika Afisi yako, ili apatiwe sheria yote ili aweze kuelewa zaidi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nahisi utaratibu ambao umefuatwa hivi sasa na ni utaratibu sahihi kwa Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu. Nafikiri kwa taarifa hiyo haina haja ya kuakhirisha kwa sababu hiyo. Labda kuwe na sababu nyengine ambazo Mhe. Spika, unaweza ukazikubali au ukazikataa. Nakushukuru.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tuna tatizo kidogo naomba niseme maneno hayo kwa sababu chombo hiki Waheshimiwa Wajumbe tunatakiwa tuwe makini sana, tuko makini naamini hivyo lakini tuzidishe umakini wetu. Mimi ninaikumbuka hii sheria ilivyo ni *volume* kubwa kweli, sasa tunaporekebisha sheria na tukasema *volume* zile tuzitengeneze tena tuzilete humu ndani, kwanza tuelewe kuchapisha hivyo ni gharama ya mara ya pili sawa sawa na ule mswada ulivyokuwa mwanzo ulivyoletwa basi gharama zile tuzirejee tena. Lakini kama mswada huu tumekuwa nao kwa kiasi cha miezi mitatu hatukuweza kufanya chochote, mwezi wa Oktoba mwaka jana miezi mitatu karibu mpaka kuingia Januari, hivi tukiakhirisha muda mfupi tutafanya nini?

Huko nyuma tulikuwa tunategemea siku 21 Kamati inakaa inamaliza pengine kama jana tu mambo yote yanaletwa hapa lakini hii tuna wasaa wa muda mkubwa sana Kamati kuweza kufuatilia na Wajumbe kuweza kufuatilia. Kwa sababu miswada inapowasilishwa mezani husomwa kwa mara ya kwanza. Miswada yote ile Waheshimiwa Wajumbe wote tunapata, tunakuwa nayo, tunarudi majimboni, Kamati inayohusika inafanya kazi yake, wanaita wadau lakini Waheshimiwa Wajumbe pia na sisi tuna nafasi yetu kila mmoja kuweza kufanya kazi ya utafiti kama Mhe. Waziri wa Katiba alivyofanya, na madhumuni ilikuwa ndio haya. Mswada turejeshe utaratibu, kwa sababu utaratibu ulikuwepo huko nyuma kusomwa kwa mara ya kwanza kwa kuwasilisha lakini mjadala wake uje kwenye mkutano unaofuata. Sasa *volume* yenyewe ndio hii sasa hebu niambieni *volume* hii ina kurasa 297 tukishaitawanya kote wote Waheshimiwa Wajumbe hii, *fund* hiyo itoe Baraza la Wawakilishi, vikao vijavyo ndio havipo kwa sababu Waziri atakacholeta kuniletea hii moja *actual* hata hana haja kuleta tunazo.

Sasa hii iweze kutawanywa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote, hapana, tunategemewa tuwe makini katika matumizi, tunategemewa tuweze kufanya shughuli zetu kwa umakini kwa kuangalia kitu ambacho kinategemewa kiwasilishwe kwenye mkutano ujao kwa namna ile ambayo tunasoma kwa mara ya kwanza kwenye mkutano uliopita. Sasa mimi nafikiri hilo

Waheshimwia Wajumbe tukubaliane. Ninajua tunapokuwa na sheria ambayo ni mpya kwa mara ya kwanza serikali huwa tunaiomba itufanyie semina kwa kutafuta uelewa, lakini sheria hii ilikuwepo tunafanya marekebisho. Huku nyuma tulikuwa kitu hiki hatuna tumeamua kuwa na cha kwetu *volume* yenyewe ndio hii kama tunavyoiona.

Sasa mimi nadhani tukubaliane kwamba hoja hii iliyowekwa na Mhe. Omar Ali Shehe na kuungwa mkono na Mhe. Asha Bakari isitupeleke tukaweka utaratibu ambao hautakuwa na manufaa kwa chombo chetu *actually* itakuwa ile haja tuliyoifanya huku mapema haipo kusoma mswada mara tatu, wa kwanza inawasilishwa inakuwa taarifa kwa Waheshimiwa Wajumbe, inakuwa taarifa kwa umma. Wajumbe sisi ndio Wawakilishi kwenda kwa watu wetu, kama kuna mtu ana maoni basi atatoa anaweza hata kuitisha mikutano ndani ya jimbo au kwa kundi la watu ambao wanahusika kama vile Kamati ilivyokuwa imeita wadau.
Waheshimiwa Wajumbe tusiweke utaratibu ambao hatimae utafanya chombo chetu hiki na pengine wizara kwa jumla kutumia isivyo sawasawa na wala hailazimiki kufanya hivyo, kazi yetu kubwa ni sisi kujituma, kurudi katika ofisi yetu hapa *library* na mswada wako ule ambao unahitaji marekebisho ukafuatilia vifungu vile ambavyo vinahitaji marekebisho. Lakini zaidi ya hivyo Waziri amewasilisha kitu ambacho kisaidie hayo, mimi nadhani niwaombe radhi sana Waheshimiwa Wajumbe hili jambo tuendelee na uwe ni utaratibu wa kuelewa kwamba tunaposoma miswada kwa mara ya kwanza maana *at least* ingekuwa ni mswada wa dharura hilo suala jengine lakini huu haukuwa mswada wa dharura umefuata utaratibu wake kama ulivyo, tujitume kufanya kazi za wananchi.

Waheshimiwa Wajumbe nakuombeni sana na nakutakeni radhi sana tuendelee. *(Makofi*). Kama kuna michango kama hakuna tumuite Mhe. Waziri afanye majumuisho.

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla:** Ahsante Mhe. Spika, nadhani Wajumbe walizubaa kidogo kwa sababu kuna barua tulipewa na Baraza ambayo ilikuwa inaonesha wakati huu tulikuwa na programu nyengine kuna mabadiliko au vipi pengine sijui lakini kwa sababu Mhe. Spika, hujasema kitu kuhusu programu hiyo, na kwa sababu tuna kazi ya kufanya hapa Barazani kwa mujibu wa orodha wa kazi za leo, basi mimi naomba nitumie fursa hii kama kuwapa muda wenzangu wajitayarishe niseme machache kuhusu hoja ilioko mbele yetu.

Mhe. Spika, mswada huu umekuja wakati muafaka sana, tutakumbuka miezi ya hivi karibuni tulipata majanga makubwa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwa kuwapoteza wenzetu wengi katika kadhia hizo za usafiri wa baharini. Kitu ambacho kwa kweli hakuna katika visiwa hivi ambao misiba ile haikumgusa kwa njia moja au nyengine. Kufuatia matukio yale Mhe. Spika, Wajumbe wako wengi walisema maneno mengi na pengine na walithubutu hata kutoa makemeo makali kwa serikali. Sasa mswada huu basi unaonesha kama ni miongoni mwa juhudi za serikali katika kulifanyia kazi suala la usafiri wa baharini ili mambo yaende kwa ufanisi zaidi. Sasa mimi binafsi naipongeza sana serikali kwa kuleta mswada huu ambao nadhani kwa kiwango kikubwa utaweza kudhibiti hali halisi ya usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, wawekezaji wetu walitumia ukimya huu ambao ulikuwepo kwa kweli kuleta meli ambazo hazimo katika mfumo mzuri wa kusafiria abiria hasa tukilinganisha na bahari yetu ambayo ni bahari pevu yenye maji makali, yenye kina kikubwa, bahari yenye mawimbi makubwa, meli nyingi ambazo zimetumika kuwachukua wananchi kuwapeleka kutoka kisiwa

kimoja hadi chengine, kwa kweli zilikuwa hazina sifa na si aibu kusema serikali iliyanyamazia kimya kwa muda mrefu. Sasa mimi nashukuru mswada huu umeletwa na utaweza kubadilisha mwenendo wa uwekezaji katika mambo ya usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwenye marekebisho ya kifungu kwa mujibu wa mswada huu ni kifungu cha 12 lakini marekebisho ya kifungu cha 17, hichi kifungu cha 12 kinasema sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 17 (a) mara baada ya kifungu cha 17 kama ifuatavyo:

Kifungu chenyewe kinasema hivi, hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo Zanzibar.

Mhe. Spika, marekebisho haya yanaweza yakatufanya tuwe na vyombo vichache sana vitakavyo-*qualify* kuchukua abiria, ukitizama kwa undani sana utakutia meli ya MV Maendeleo hapa itakuwa haifai tena, Serengeti itakuwa haifai tena na hata Ukombozi haichukui abiria lakini pia nakumbuka huku usoni kuna kifungu ambacho kinampa Waziri kutunga masharti ya meli za mizigo nazo.

Sasa hii mimi naipongeza sana serikali kwa sababu najua katika kipindi cha mpito tutapata tabu sana. Maana yake ukishaifanya Maendeleo isifanye kazi na halafu unaweza kujiuliza sasa tuifanye nini lakini ukishaifanya na Serengeti isifanye kazi, basi tutakuwa na kipindi kigumu kidogo. Lakini mara nyingi ukitaka kurekebisha mambo lazima usiwe na muhali na kwa hili mimi serikali naipongeza sana. Siku nyingi nilikuwa ninasema mimi baada ya matokeo ya ajali zile zilizotokea, halafu tukaangalia na utuuzima wa meli hasa ya Serengeti, nilikuwa nikisema sana kwamba meli ile wakati umeshafika wa kuizuia isifanye tena kazi hasa kwa abiria. Kwa sababu ile kwa wanaoijua kule chini wanasema ile meli hali yake ni mbaya sana, mapleti yake yameshaoza, yamezibwa zibwa kwa saruji. Wengine wanakwambia kule chini kuna mtu kaajiriwa *special* ana mashine ile ya *water pump* ya kutoa maji wakati meli ile inakwenda basi ile mashine inafanya kazi ya kutoa maji yanayovuja kwenye meli kuyatoa nje.

Sasa tukiangalia Mhe. Sspika, ajali zilizotokea katika nchi yetu, watu tuliowapoteza halafu tukawa na meli inakwenda katika msingi huo kwa kweli riski kwa asilimia 90 haifai kabisa. Sasa mimi ninafurahia sana kifungu hiki na ninamuomba sana Mhe. Rais mara tu baada ya sheria hii kupitishwa basi asichukue muda aitie saini ili tuweze kukwepa majanga ambayo tunayafikiria yanaweza yakatokea tena kwa mara ya tatu. Lakini wakati huo huo basi niiombe serikali pamoja na mkakati wetu mkubwa wa bajeti tulioupitisha mwaka huu basi serikali iwe inafuatilia kwa haraka zaidi upatikanaji wa meli nyengine, kwa sababu ukishaitoa Maendeleo na Serengeti kwa hivyo ule mchakato uendelee kwa *speed* ili *replacement* ifanyike haraka.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika kifungu kidogo cha tatu kutoka ile 17(a) 1 nije kwenye 17(a) 3. Mhe. Spika, tukiangalia ile ajali ya pili ya MV Skagit ilitokea kwa sababu ile meli ilikuwa imebadilishwa maumbile yake, na hii inawezekana kwa sababu ya tamaa ya wawekezaji lakini yule *engineer* aliyeitengeneza ile meli aliiweka katika kiwango kile kwa kuangalia uwezo wake katika kuhimili mawimbi ya baharini. Sasa inasemekana ile meli imeongezwa ilipigwa tena ghorofa moja tena juu ikawa refu kwa kwenda juu lakini *base* yake huku chini nyembamba. Kwa

hivyo ilipopata misukosuko ya mawimbi ikawa rahisi kulala chini. Sasa kifungu hiki cha tatu nafikiri nikisome kidogo. “Hakuna meli itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa madhumuni ya kuchukua abiria ndani ya Zanzibar ikiwa meli hiyo imebadilishwa kutoka katika asili ya utengenezaji wake”. Na ukiangalia maelezo yaliyoko chini kwa madhumuni ya kifungu hiki mabadiliko maana yake ni mabadiliko yoyote yatakayobadili muundo wa meli kutoka katika uhalisia wake kama vile ukubwa, upana, kina cha kufungia, mashine za umeme vyombo vya mawasiliano, wingi na vitu vya  aina hiyo.

Sasa hii ni muhimu sana hata hizi zilizobakia zina mabadiliko ya namna hii kwa mfano kama hizi mashine za umeme, meli hizi tunazochukulia abiria Mhe. Spika, nyingi mashine zake za asili zimekufa na matokeo yake wameweka vi-*generator* mule ndivyo vinavyozalisha umeme wa kuendeshea meli vi-*generator* ambavyo havina uwezo sawa sawa na zile mashine zake za asili meli kubwa inawekwa ki-*generator* kidogo. Matokeo yake mara unasikia injini moja haiendi, mara hivi, mara hivi. Kwa hivyo hii italinda utaratibu.

Na ninachokiomba Mhe. Spika, unajua wazanzibari tuna tabia moja, tuko mbele sana wazanzibari katika kutunga sheria, siku zote nasema hivyo lakini Mhe. spika, tukishatunga sheria tunazifungia makabatini hazitekelezwi na hili ni tatizo moja kubwa sana na kwa tabia hii Mhe. Spika, hatuwezi kubadilika wazanzibari lazima hii tabia tuiache. Mimi huwa mara nyingi ninatoa mfano mmoja tena ninautoa kwa sababu unanikereketa sana katika nafsi yangu. Tulitunga sheria miaka ya nyuma hapa ya kuwadhibiti watu wanaowaadhibu wanyama, sheria ipo humu Barazani tumeshaikumbusha zaidi ya mara tano, sita, lakini Mhe. Spika, bado sheria ile mpaka leo haijafanyiwa kazi hata kwa asilimia moja tunawaona wanyama wanaadhibiwa. Mtu anachukua punda yule anamuweka gari halafu kama mtu na huruma zako utaona machozi yanakutoka. Mtu anatumia kilomita nzima kumpiga yule punda magongo mpaka yule punda ule mwili unakufa ganzi hana la kufanya. Serikali ipo, sheria imetungwa, askari wamezagaa barabarani hakuna mtu anayechukuliwa hatua. Mara moja niliuliza watu wangapi wameshtakiwa kuwaadhibu wanyama sikupata jawabu mpaka leo.

Sasa na hii sheria tunaitunga hii lakini usije ukashangaa Mhe. Spika, tumeshatunga sheria nzuri kama hii Rais keshaweka saini lakini utakuta mambo haya ambayo tumeyakataza humu bado yanaendelea na serikali bado inaendelea kuwatizama. Sasa naomba sana hii sheria tunayoitunga basi tufike pahali tuifanyie kazi, wenzetu ndio wanavyofanya duniani wanaheshimu *principles* na sheria zao. Na tukiwazowesha watu hivyo tutakwenda vizuri. Mhe. Spika, hata ukizungumza habari ya barabara serikali inakwenda inapima eneo la barabara inaweka bikon za barabara lakini watu wanakuja wanajenga mule wanazivunja zile bikon na serikali ipo inatizama tu. Siku moja wakitaka kupanua barabara sasa wanalazimika kutoa fidia kuvunja nyumba za watu ambao ziko ndani ya bikon mwa barabara. Huu ni mfano mwengine kwamba sheria tunazozitunga hazifuatwi. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Spika, kazi moja ni kutunga sheria lakini kazi ya pili kubwa ni kufuata sheria zetu tunazozitunga ili mambo yaende sawa.

Mhe. Spika, kifungu cha 13 cha mswada huu kinasema sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18 mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo:

“Waziri anaweza kutunga kanuni zitakazoeleza ukomo wa umri wa meli zisizokuwa za abiria kusajiliwa na kupewa leseni Zanzibar”. Sasa hii ndio niliyoisema hii kwamba zile meli za abiria

zimeekewa miaka 15 na kifungu hiki kizuri sana kinampa Waziri uwezo wa kutunga kanuni kwa ajili ya kuweka ukomo wa meli wa kuchukua mizigo. Ni kweli kwa sababu hata kama ni mizigo hamna roho za watu lakini mna mali za watu, kwa hivyo nayo ni muhimu kupatiwa kanuni kwa ajili ya kudhibiti sio mameli mabovu yachukue tani kwa tani ya mizigo ya watu halafu waizamishe baharini. Nilikuwa naomba sana katika kuzingatia hili basi Mhe. Waziri azingatie pia muundo wa ile meli yenyewe inayofaa hasa kutembea katika maji ya Zanzibar.

Mhe. Spika, maji yetu au bahari yetu ya Zanzibar ni bahari yenye mawimbi makali, mameli yanayochukulia mizigo na abiria katika bahari hii mara nyingi wanakwenda kutafuta mameli ambayo huko kwao yamezoea kutumika mito ambayo haina mawimbi, haina kina kikubwa ndizo zinazokuja hapa ndio zikapewa uwezo wa kuchukua abiria na mizigo ya watu katika bahari yenye kina kikubwa kama Nungwi. Wataalamu mimi si mtaalamu wa mambo ya *marine* lakini wataalamu wanasema meli zile haziruhusiwi huko kwao, yaani meli isiyokuwa na mkuku hairuhusiwi kupita katika bahari yenye mawimbi makali. Lakini hapa bado yapo, kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri katika kutunga kanuni sijaangalia vizuri kama kuna kifungu kinazungumzia jambo hilo, lakini kama hakimo si wakati wa kutunga kanuni pia aangalie meli za *land craft* bwana kwa bahari ya kwetu hazifai Mhe. kabisa na zipo nyingi na hata ile kubwa tunayoisifu kweli kweli ile mpya kubwa iliyokuja juzi ambayo sasa ndio kwa kweli inakamata nambari moja kwa kuchukulia abiria nalo ni *land craft. Thanks God* bahari haijachafuka lakini siku bahari itakayochafuka basi kwa kweli hali itakuwa mbaya. Nilikuwa naomba sana wakati wa kudhibiti mambo haya basi meli lazima ziwe na mkuku, meli za *land craft* bwana hazitufai Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nilisema nasema kidogo ili kuwapa wenzangu nafasi ya kujitayarisha mimi niliyoyaona ya haraka haraka ni haya lakini wenzangu watakuwa wameona mengi zaidi na kwa hivyo mimi nataka niseme tu kwamba ninaunga mkono sana kwa asilimia mia moja mswada huu, kwa sababu utaweza kuepusha hasara nyingi ambazo tungeweza kuzipata wazanzibari kwa mameli yasiyokuwa na uhakika.

Baada ya hayo naomba kukushukuru tena halafu nikae kitako.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia mswada huu ambao ni sheria ya marekebisho ya usafiri wa baharini. Awali ya yote kwanza nimshukuru *Subhanahu wataala* aliyetujaalia uzima na afya na kuweza kufanya harakati zetu za maendeleo za kila siku.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii adhimu kuipongeza Wizara ya Miundombinu kwa kutuletea sheria hii leo hii katika Baraza letu. Mhe. Spika, sisi sote ni mashahidi wa kutosha tulioshuhudia matukio ambayo yalileta huzuni katika taifa letu mawili makuu ambayo yalitokea katika kipindi kifupi sana, tofauti yake ilikuwa ni kipindi kifupi. Kwa kweli matukio yale yalitia majonzi makubwa taifa letu na leo tumeona namna matukio yale yalivyoweza kusaidia katika kurekebisha sheria hii ya kupata usafiri ambao utakuwa ni usafiri wa salama.

Mhe. Spika, mimi labda niseme kuwa kuna sababu nyingi ya kuwa sasa hivi tuwe makini katika usafiri wetu wa baharini, hasa tukizingatia kwamba harakati zetu za kiuchumi zimezidi watu

wengi wamekuwa wakitumia usafiri wa baharini kwa sababu wanatumia katika shughuli mbali mbali za kiuchumi zinazowaletea tija katika mapato yao.

Lakini vile vile idadi ya watu imeongezeka kwa kasi kwa hivyo mahitaji yamekuwa makubwa. Vile vile sekta yetu ya utalii imekua kwa hivyo sio kwamba tunatumia sisi tu, vipando hivyo, lakini na wenzetu wageni wanavitumia vipando hivyo.
Kwa hivyo, mimi nafikiria kwamba sasa kwa kweli ni wakati mwafaka wa kuiangalia kwa makini sana sheria hii ili tuhakikishe kwamba usafiri wa baharini unakua ni wa salama na utawafikisha wale wanaotumia katika maeneo wanayokwenda kwa usalama.

Mhe. Spika, mimi naanza moja kwa moja katika ukurasa wa 285, katika kuipitia sheria hii katika ukurasa huo kifungu cha 10(2) kinasema kwamba, "mtu yeyote atakaevunja masharti ya kifungu kidogo cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atahukumiwa kwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua dola elfu tano. Ninavyojua mimi kwa kawaida ikiwa atashindwa kulipa fedha za adhabu ile basi ina maana kwamba kutakuwa na kifungo, lakini hapa sijaona kwamba kama kutakuwa na kifungo. Sasa ningeomba hapa kitajwe kifungo ambacho mtu yule akishindwa kulipa fedha zile ikiwa amefanya makosa.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye kifungu nambari 12 ambacho kinasema "meli itakayokuwa na sifa ya kusajiliwa chini ya kifungu cha 9 lazima ikidhi matakwa ya kijifungu kilichotangulia. Unajua mara nyingi lugha inayotumika ya kisheria inakuwa kidogo imejibanabana, tumekuwa na maombi ya mara kwa mara kusema kwamba hebu tuifanye hii lugha ya sheria sasa hivi iwe *friendly user*, kila mmoja anapoisoma aweze kuifahamu. Nafikiria hapa badala ya kusema kwamba lazima ikidhi matakwa ya kijifungu kilichotangulia kwa nini isiseme lazima ikidhi matakwa ya kifungu a, b au c ili mtu aki-*refer* anajua ana-*refer* kitu gani. Mimi ni ushauri wangu huo.

Sasa niende kwenye kifungu cha 12(3) ambacho kinazungumzia uasili wa meli pamoja na mabadiliko yake. Mhe. Spika, tumeona hapa mara nyingi sana vipando vyote sio meli tu, hata gari zikija hasa zile za biashara kunaongezwa vitu, wafanyabiashara wanaongeza ili kuongeza mapato yao. Tunaona katika daladala basi linakuwa ni la watu 18 lakini linaongezwa viti mpaka vinakuwa 24, lakini mara nyingi inakuwa hatujui hatari yake ni kitu gani.

Mimi kwa kweli kifungu hiki kimenifurahisha sana isipokuwa natoa tahadhari tu, kwa sababu kinasema kwamba, "kwa madhumuni ya kifungu hiki mabadiliko maana yake ni mabadiliko yoyote yanayobadili muundo wa meli kutoka katika uhalisia wake kama vile ukubwa, upana, kina cha kufungia mashine ya umeme, vyombo vya mawasiliano, winji au vitu vinavyofanana navyo". Wasi wasi wangu mkubwa meli hizi zinakuwa na idadi maalum ya viti, vitanda zinapokuwa huko zinakotoka kwenye uasili wake, wasi wasi wangu mkubwa kwamba hata hivi viti na vitanda vinaweza vikaongezwa. Kwa hivyo, naiomba wizara iwe makini katika hilo pia kwamba litiwe kwenye sheria, kwamba hata umbo lake la ndani kuongezwa kwa vitu kama hivi viti ili uongeze idadi ya abiria basi hili pia ni kosa na naomba sana litiwe katika kifungu hiki ili kuainishwa kuwa na hili pia halitakiwi kuwepo.

Mhe. Spika, baada ya hapo nakwenda katika kifungu cha 17(4) ambacho kinasema waziri anaweza kutunga kanuni za usajili sambamba na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe.

Spika, mimi mara nyingi huwa napata tabu, nikitazama sheria za Kiingereza halafu nikitizama na za Kiswahili halafu nikitafsiri neon kwa Kiswahili kidogo linanipa tabu hasa kwa kuwa si mwanasheria mimi. Lakini unaposema waziri anaweza nimetizama katika sheria ya Kiingereza nimeona *may* yaani anaweza waziri kutunga sheria. Sasa neno "anaweza" mimi huwa linanitatiza kwa sababu anaweza atunge anaweza asitunge sheria. Vile vile kuna neno '*shall'* ambalo kwamba anatakiwa atunge sheria, sasa hapa kidogo labda waziri anaweza kuja kunifahamisha kwa lugha ya kisheria.

Kwa sababu tatizo linalojitokeza mara nyingi sana kwanza mara nyingi sheria nyingi tunazitunga hapa lakini zinachukua muda sana kwa kutungiwa kanuni pengine zinaweza kuchukua hata miaka miwili. Tunapokwenda kwenye kamati sehemu nyengine tunaambiwa hazijatungwa kanuni, kanuni hazijafikishwa, kanuni ziko BLM kila siku tunaambiwa neno kuhusu kanuni. Sasa hapa kwanza kumpa uwezo waziri anaweza au anaweza asitunge anavyotaka mwenyewe, sheria inasema anaweza lakini anaweza akasema siwezi kutunga naweza nikakaa hivi hivi bila ya kutunga sheria.

Kwa hivyo, hapa mimi naomba tuseme waziri atatunga kanuni za usajili na nafikiri neno hilo hilo limejirudia katika kifungu cha 27(2) ambacho kimesema, 'mamlaka inaweza itunge kanuni'. Sasa mamlaka pia tunasema inaweza kutunga, mamlaka inatakiwa itunge kanuni za hatua za kinidhamu na kuweka adhabu kwa mabaharia watakaokiuka masharti ya usalama, nafikiri hivyo ndio itakuwa sawa zaidi kuliko kusema anaweza kwa sababu sio lazima.

Mhe. Spika, nakwenda katika kifungu cha 25(2) ambacho kinazungumzia kwamba ikiwa kile kipando yaani meli imekwama na mamlaka ya umma itaitoa ile meli hiki kifungu kidogo kimenitatiza. Kwa sababu nafikiria mimi ikiwa ile Mamlaka ya Umma imetumia gharama ya kuitoa ile meli pahala ambapo imenasa na wakifanya mauzo je, ile meli ikiwa kwamba ni mbovu haiwezi tena kufanya mauzo ya aina yoyote *return* zile zitatoka wapi? Sijui kama waziri amenifahamu vizuri. Lakini ninachokusudia ni kwamba, ikiwa kama Mamlaka ya Umma itagharamika katika kuikwamua ile meli na meli ile itakapokuja sasa kwenye maji itashindwa kufanya kazi za kupata mapato je, ile gharama atagharimia nani?

Sasa mimi ninavyofikiria kwamba mara nyingi sana vyombo hivi vinakuwa na bima, hilo ni suala la kwamba wizara iangalie kuwa bima ile waliyonayo meli ile ilipwe mamlaka badala ya kwenda kwa yule ambaye anahusika aliyeikata kwa meli ile.

Mhe. Spika, mimi nafikiri katika vifungu hivi kwa sheria hii nadhani nimemaliza, nashukuru sana kwa kutuletea mezani sheria hii na mimi naamini kwamba uwezekano kwa kuwa tumeitunga sheria hii kwa kipindi hiki ambapo uwezo mkubwa tunao wa kufanya haya mimi naomba sana tuwe *serious* katika utekelezaji wa sheria zetu.

Tatizo moja mwenzangu aliyetangulia amelizungumza hapa ni tatizo ambalo mara nyingi sana linafanya mambo yetu yasiende. Kwa sababu hatutekelezi ipasavyo sheria zetu, tunakiuka sheria zetu kwa sababu ambazo si za msingi. Mimi namuamini sana waziri aliyeko sasa hivi na naamini kwamba ana uwezo wa kutosha wa kusimamia wizara yake katika kusimamia sheria ambazo zimetungwa na Baraza la Wawakilishi na ambazo zimepitishwa na Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba utekelezaji wa sheria hii uwe makini na Mwenyezi Mungu atunusuru na jengine lolote baya kutokea, kwa sababu tutakuwa na sheria na yule ambaye atavunja sheria tutajua sheria inasema imfanye nini. Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono mswada kwa asilimia mia moja ahsante sana nashukuru.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusu sheria iliyopo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kwanza niipongeze serikali kwa kuweza kuleta marekebisho haya. Kwa kweli marekebisho haya Mhe. Spika, yamekuja wakati muwafaka na watu wameona karibu tu hapa kwa hizi ajali mbili, lakini Mheshimiwa marekebisho haya yalitakiwa yaletwe tangu mwaka 1991 wakati pale ilipozama ile Boti ya MV. Kabul ambayo iliuwa watu wengi mno, lakini leo imekuja tunashukuru na tunaipongeza serikali.

Mhe. Spika, sheria au marekebisho yoyote ya nchi lazima yaende sambamba na mazingira halisi ya nchi ile. Kwa mfano hapa Zanzibar zaidi ya asilimia 80 ya Wazanzibari tunaitegemea bahari kwa ajili ya safari zetu. Kwa hivyo, sheria za nchi lazima ziwe makini mno katika kusimamia usafiri wa baharini kwa hapa Zanzibar. Sasa Mhe. Spika, katika hili niendelee kuipongeza serikali kwa kuweza kuleta marekebisho haya ambayo naamini kwamba yatasimamia vyema vyombo vya usafiri baharini pamoja na kuondosha usumbufu wa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi naona kuna mapungufu matatu katika sheria hii. Moja ni kwamba sheria imejikita zaidi katika usajili wa vyombo, usajili wa mabaharia, lakini haikuangalia sana jinsi ya marekebisho na kuimarisha vyombo vinavyoongoza hivi vyombo vya baharini ikiwemo minara pamoja na maboya. Mhe. Spika, kama kitu cha kuangalia, kama kuna kitu cha kuwa makini katika kusafirisha watu baharini ni pamoja na kuimarisha minara pamoja na maboya. Kwa sababu wale mabaharia wetu mara nyingi wanaelekezwa na mambo yale, la kusikitisha minara yetu mingi hapa haifanyi kazi. Hata hivi juzi nilizungumzia hapa mnara uliopo Kaskazini Unguja na lile *turning* boya liliopo Mkoani yalikuwa hayawaki kabisa. Sasa ile ni hatari, ni tatizo ambalo linaweza likasababisha matatizo makubwa baharini.

Kwa hivyo, namuomba waziri katika hili sheria hii isimamie mamlaka itayohusiana na vyombo vinavyoongoza meli sio kuviachia achia tu minara haiwaki, maboya hayawaki tukawaachia achia tu hawa wakatusababishia ajali, meli zinaweza kugongana, zinaweza kuingia kwenye mwamba na kusababisha vifo. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, katika hili sheria hii ijikite isibu katika mambo ya kuimarisha minara pamoja na yale maboya yanayoongoza meli baharini. Hili ni pungufu moja Mheshimiwa.

Pungufu la pili Mhe. Spika, inaonekana waziri hakukaa kwa sababu lengo la sheria ni kuondosha usumbufu kwa wananchi na kurahisisha usafiri wa baharini kwa sababu asilimia 80 ya Wazanzibari tunatumia bahari, ilikuwa Waziri huyu wa Miundombinu na Mawasiliano aende akakae na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wapange vizuri kuhusu kuondoa usumbufu baharini. Hivi sasa Mhe. Spika, wasafiri wa baharini wana usumbufu mkubwa kwa sababu huwezi kupata tiketi pale kama huna kipande cha *Zan ID* na waziri hakwenda kukaa na waziri mwenzake wakaondoa matatizo haya ili watu wasafiri vizuri baharini, sasa watu wanakwenda wanakosa tiketi kwa sababu hawana vitambulisho vya *Zan ID*, wanalazimika kununua tiketi za kulangua, kwa sababu mwenye *Zan ID* anakwenda kununua

tiketi nyingi huyu hana anamuuzia tiketi za kulangua, huu ni usumbufu na ni mapungufu makubwa sana ya sheria hii.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama anataka kweli atuondoshee usumbufu basi ende akakae na maulana huyu bwana mwenye *twayyibu- l-asmai* katika siasa za nchi hii Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Bwana Mwinyihaji Makame wawatatulie wananchi tatizo la *Zan ID* ili wakenda kukata tiketi za kusafiri baharini waweze kupata habari hizo. Hilo ni pungufu jengine.

Mhe. Spika, niende katika kifungu Nam. 12 cha hii sheria, kifungu hiki kwa heshima yako na unyenyekevu wa hali ya juu Mhe. Spika, naomba uniruhusu nikinukuu.

Kifungu Nam. 12 kinasema kwamba,

> "Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 17a mara baada ya kifungu cha 17 kama ifuatavyo:
>
> 17a. (1) Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake, itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo Zanzibar"

Mhe. Spika, nia ya serikali naamini ni nzuri katika hoja hii, lakini sheria yoyote nimesema lazima iende sambamba na mazingira ya nchi hii nchi ni masikini, mimi naamini umadhubuti wa chombo unategemea zaidi *service* ya vyombo hivyo na sio umri wa kutengenezwa kwake. Mhe. Spika, sisi katika miaka ya 1970 tulikuwa na meli hapa ambazo meli hizi zilitengenezwa tangu katika miaka ya elfu moja mia nane mwishoni mwishoni hivi, M.V. Afrika na M.V. Jamhuri. Meli hizi sisi tulizirithi kutoka kwa Wakoloni na zilikuwa zikitumia makaa hapo mkaa wa mawe ilikuwa hawatumii hata haya mambo, lakini mara baada ya kuzipata zile meli aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano siku zile Marehemu Pili Khamis Mwenyezi Mungu amrehemu sana huyu bwana aliamua zile meli kuzishughulikia kwa *service,* tulizifanyia *service* na tukazitoa katika mfumo wa mkaa wa mawe tukaingia katika matumizi ya *diesel*, Mhe. Spika, meli zile katika mwaka 1800 mpaka juzi juzi hazikuzama ziliyayuka tu pale baharini wala hazikuzama zikauwa watu, kwa sababu sisi katika Afro Shirazi tulizisimamia vizuri katika *service* na zikasafirisha watu vizuri sana. Leo unaposema miaka 15 mheshimiwa hivi vyombo bado ni vipya, unataka kui *monopolise* hii *business* ya baharini kumkabidhi tajiri mmoja.

Mhe. Spika, kwenye *showroom* hizi za magari hapa kuna magari yametengenezwa miaka 20 mpaka 25 na ndio tunayonunua na kutembelea sisi wengine. Sasa napata wasi wasi marekebisho haya ya kifungu hiki kikija kikihamia katika usafiri wa nchi kavu wengine tutakuwa tunatembea kwa miguu, kwa sababu hatuna uwezo wa kununua gari mpya na hizi meli Mhe. Spika, miaka 15 bado ni mpya na zinapatikana kwa bei mbaya huko kwao, jambo ambalo pengine anaweza akawa Mhe. Hija Hassan tu ndiye anayemiliki usafiri wa baharini hapa sisi wengine tukawa hatumiliki aka-*monopolise business* ya bahari na matokeo yake ikawa ni tatizo.

Mimi nashauri tu kwamba angalau meli hapa isipate usajili kuanzia miaka 25 na kusimamia ZMC iwe na technical monitoring team kuweza kufanya sana checking kipindi baada ya kipindi

na kisizidi baada ya miezi sita meli zote hapo nadhani tunaweza tukasaidia sana watu kuweza kupata vyombo vingi na ajali zikapungua, lakuweka miaka 15 haki ya Mungu atakuwa ni mfanyabiashara mmoja tu ndiye anayemiliki usafiri wa baharini lakini wengi hawataweza kumiliki hivyo vyombo.

Mhe. Spika, niende katika kifungu nambari 13 naomba nacho nikinukuu.

Kifungu Nam. 13 kinasema:

> "Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo:

Kanuni:18A Waziri anaweza kutunga kanuni zitakazoeleza ukomo wa umri wa meli zisizokuwa za abiria kusajiliwa na kupewa leseni Zanzibar"

Mhe. Spika, katika hili waziri tusimuachie hii kazi, hii kazi ni lazima ifanywe na sisi kama ilivyo katika hiki kifungu cha 12 kwamba sio tuweke ukomo, hapa sheria inapendekeza miaka 15 lakini na hapa vile vile hivi vyombo vya mizigo visivyokuwa vya abiria navyo ipendekezwe tutajiwe tuipitishe hapa. Kwa sababu tukimpa waziri meli zinawezakuwa ni mbovu akenda akafanyiwa *lobbying* huko na jamaa akampitishia tu, lakini kuja kuli-*lobby* Baraza hili sio rahisi. Tusimpe mtu mmoja hii kazi bwana, kazi hii tusimpe waziri ya kuhusu vyombo vya abiria na mizigo, ile mizigo inatumika kwa fedha za serikali, inanuliwa kwa fedha za serikali na pengine inaweza kuwa sio mizigo ya wafanyabiashara tu wa *private* inaweza kuwa na mizigo ya serikali ikajakuwa pesa za serikali tunazipoteza kwa vyombo vibovu lazima navyo tuviwekee ukomo sisi tusimuachie waziri kwa kanuni iwe ni sheria hasa iseme, vyombo vya mizigo visisajiliwe mpaka vitimie umri huu.

Mhe. Spika, nina hoja kwa sababu sisi hawa wafanyabiashara mizigo yao ikazama tutakosa mapato serikali na sisi serikali tunatia mizogo yetu ikizama nayo ni tatizo vile vile kwa hivyo, lazima tuweke ukomo sisi.

Mhe. Spika, mimi leo nilifikiri hakuna Baraza kwa ile barua tuliyopewa nikasema kunai le mafunzo ya katiba wala sijajitayarisha nilikusudia kuja kuchangia kesho. Kwa sababu barua imetupoteza sana ile tuliyopewa, mimi nilikuwa nafikiria sasa hivi tuko kwenye mafunzo ya katiba, lakini kwa mnasaba huo hizi nyalio nilizokwishakuzitia zinatosha.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika, nami kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu unaozungumzwa, lakini kwa mshangao mkubwa na masikitiko ni mswada wangu wa mwanzo kuuona wa ajabu kabisa. Kwa sababu kinachozungumzwa hapa ukenda kuangalia huko bandarini hakuna ofisi inayoongoza. Mwaka jana nilipiga kele ile ofisi ya *Signal Tower* haipo, sizungumzi kwa kubahatisha waziri akijakunambia kanioneshe hiyo ofisi ya meli inayoongoza mamlaka hiyo *signal tower* imeporomoka, sasa hivi ofisi iko katika mkoba wa ukili ikifika usiku si kwa kubahatisha ni kwa kuyaona kama atakuwa tayari Mhe. Waziri akanioneshe. Leo tunajadili kitu kuuziana paka kwenye gunia wakati hujamuona mswada huu una maana gani, tunaleta mswada tunajadili kitu wananchi wanatusikiliza wakati kitu cha kuongozea hakipo mswada huu sijui una *interest* gani maana yake, sijui unatupeleka wapi.

Sisi tunaletewa msaada wa meli hicho chombo cha kuongozea meli hakipo bandarini, jumba limeporomoka lile nililipigia kelele ikawa inatiwa *lipstick* ikapakwa, ikaanguka matokeo yake kikaonekana nilichokizungumza. Sasa Mhe. Waziri mswada huu unatusaidia nini, wananchi wanatusikiliza ni chombo chao muhimu leo tunaleta mambo ya ajabu hata watuelewe vipi tungetengeneza angalau ile ofisi ya kuongozea meli pale bandarini, mapesa mengi yanapotea hapa hakuna kinachokwenda tukatengeneze kwanza ile ofisi ya meli kule bandarini leo ofisi imo ndani ya mkoba wa ukili tunakwenda wapi, ni mswada wa ajabu kweli kweli. Haya sizungumzi kwa kubahatisha Mhe. Spika, mimi niko tayari akanioneshe iko wapi hii ofisi ilikohamia hivi sasa, ikifika usiku utawakuta pale wamejaza kwenye mkoba wa ukili wanachomoa funga wapi, funga wapi, wananchi wanatusikiliza leo tunajadili mswada huu tunawaambia nini.

Mwaka jana nilipiga kelele na Mwenyezi Mungu akapitisha rehema zake nyumba ile pale imeporomoka na hawajui wako wapi, leo meli tutaiongoza vipi, itaingia vipi bila ya kuwa na ofisi. Mhe. Spika, ni mswada wa ajabu unaokuja hapa.

Kama hapatoshi hapo Mhe. Spika, nije kwenye kifungu cha 17 (1), naomba nikinukuu. Kinachozungumzia ukomo wa meli, hebu Mhe. Spika, tuliangalie hili jengo lako kama hakulifanyia ukarabati linapovuja litakaa kweli hili? Nimepiga kelele kuhusu ICU nikaambiwa ipo lakini kinachofanya ICU kuwepo ni huduma. Leo ukiingia ndani chumba kitupu kile.

Leo hili jengo likivunja ukiliacha, leo Mhe. Waziri anakuja kusema miaka 15 ndio ukomo wa meli, munatupeleka wapi. Munafikiri anatakuja mwekezaji kuja kuekeza katika nchi hii? Tunawafukuza watu namna hii.

Twende hapo Kigoma Tanzania Bara kuna meli ina miaka 100 na mpaka leo inafanya kazi na wenyewe Wajerumani wanasherehekea kila inapotimia mwaka. Leo unakuja kutuletea mswada wenye kusema miaka 15, huko Ikulu wamesema miaka 20, hebu tuelezeni jamani tunafanya nini, ikiwa Ikulu imeshapendekeza miaka 20, Waziri anasema miaka 15 tukamate wapi.

Leo wataalamu hatuna hapa, huu mswada si kama wenyeviti ukakamavu wao ulikuwa umeshakwenda Bara huu, na wote umekopiwa kutoka SUMATRA, hatuna tunachokiendesha sisi. Wenyeviti ndio wakapiga kelele papatupapatu ikabaki ZMA.

Leo mwanasheria ZMA hakuna na ndiye anayetakiwa awe katibu wa kitengo hicho. Huu mswada hata bodi ya ZMA haujapitia, tunakwenda wapi. Ikawa bodi yenyewe ya ZMA ilikuwepo mswada huu hauujui, tunafanya vipi si kudanganyana huku.

Watu wanatafuta maendeleo kwa *speed* kubwa sisi tunarudi nyuma. Sasa haya sio maendeleo tunayoyatafuta. Ukomo wa meli kinachofanya huuduma ya meli wawepo na wataalamu wakague meli. Kwani hiyo gari kila mwaka kwenda kwa *Silver* kupasishwa. Sasa ikawa kikomo cha miaka 15 mimi sifahamu.

Kama kuna njia au siri fulani tuelezwe. Leo wenzetu wa Bara wanatuletea mswada huu, hebu tuangalie zile meli za kwao kule kwenye ziwa zinavyofanya kazi, na tukaangalie meli kwenye ziwa kule Mwanza inavyofanya kazi na kule hakuna bahari inavunjwa vipande ipakiwe

ikaungwe. Leo munaturejesha kule walitoka wazee wetu kupanda majahazi katika enzi za ukoloni hizo. Kwa kweli munaturudisha nyuma.

Mhe. Spika, nikiendelea hapo serikali yetu kwa muda mrefu inazingatia na kuimarisha msingi wa utawala bora. Leo kwa mshangao mkubwa tu imezuiwa bila ya kuitwa hata mtaalamu isifanye kazi ya kupakia abiria. Leo tujiulize hivyo kweli tuna akili zetu meli imetengenezwa toka kwao na asili yake mfumo wake ni kupakia abiria na mizigo unakwenda kuizuia kwa sababu gani.

Huko kutoka kwako kuna kitu kinaitwa IMO ndio international hiyo, kutoka kwao wametengeneza wazungu kitu hicho, leo anakuja mtu anasema mengine hata siwezi kusema maana hata sifahamu. Yule mzungu aliyetoka IMO ambaye ameitengeneza meli kwa abiria na mizigo, hapa anatoka mtu tu anakwambia huwezi kufanya kazi, yeye kaitengeneza meli hapa, hiyo akili kampa nani.

Mhe. Spika, nije kwenye sheria Nam. 5 ya 2006 ambayo tunaifanyia marekebisho muda huu, mimi sina meli nimeshauza kabisa…

**Mhe. Spika:** Zungumza na kiti usimjibu mtu

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Spika. Hiki kitengo kimelia na milioni 70 za kanuni ya ZMA mpaka leo kanuni haijaletwa. Kanuni hiyo mpaka leo haijafika, tunapiga kelele huku kuna meli sijui kampuni gani iliyokuwepo Dubai zaidi ya meli 45 zimesajiliwa ukiuliza hizo pesa sijui zipo wapi na serikali inapata asilimia 65. Leo kitengo kinalia kuwa hakina pesa, sasa tunafanya nini.

Mhe. Waziri unaleta huu mswada munatupeleka wapi. Tokea kuingia Barazani ndio kwanza leo nimeona mswada wa ajabu huu. Unaletwa mswada wakati chombo cha kuongezea meli kule baharini hakuna.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba serikali niipongeze kwa dhati kwa mswada huu pamoja na hayo. Lakini leo wawekezaji wadogo wadogo watakimbilia wapi. Kuna watu wameshakopa mikopo yao benki humu, unakuja mswada huu utawaweka wapi. (*Makofi*).

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba nikae kitako. (*Makofi*).

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, na mimi naomba nikushukuru kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu mfupi sana kwenye mswada huu ambao sikuwahi kuupitia kwa sababu nilidhania ungeanza kujadiliwa Jumatatu.

Mhe. Spika, nianze kwenye mswada huu nikatae sababu ambazo Mhe. Waziri amezieleza ambazo ndizo zilizompelekea kuleta mswada huu.

Mhe. Spika, kwa kadri ya upeo na uwezo wangu wa kujua Mhe. Waziri sababu hizi ambazo ameziandika si sababu za msingi. Mhe. Spika, alipokuwa akizungumza kwenye hotuba yake

amehusisha ujio wa mswada huu na matokeo ya majanga yaliyotokea hivi karibuni kwamba ndio yaliyomsukuma kuandaa mswada kwa ajili ya kusimamia usalama wa raia.

Mhe. Spika, sababu hiyo ni dhaifu kwa sababu nirejee kusema kwamba kuzama kwa meli wala hakutegemei umri wa meli, hutegemea umakini na usalama wa usafiri wenyewe. Naomba nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba mwaka 2012 meli ya MV. TITANIC ilipokuwa ikitoka Uingereza kuelekea Marekani ilizama kwenye safari yake ya mwanzo ya baharini na baada ya kuundwa tume ya Uingereza na Marekani, wote wawili walithitbitisha kwamba meli hii imezama kwa sababu ya kutofuata kwa taratibu za baharini.

Ilikuwa ni meli kubwa ya kisasa na iliyokuwa imetengenezwa kwa umakini mkubwa lakini ilizama kwa sababu ya kutokufuata maelekezo ya kitaalamu ya usafiri wa baharini. Kwa si kweli kwamba ukongwe wa chombo ndio unaosababisha kuzama.

Kwa tafsiri hiyo inaonesha Mhe. Waziri anaamini na yeye kuwa mkongwe ndiye anayekufa mwanzo, si kweli. Mkongwe anaweza akadumu na mchanga akafariki mwanzo.

Mhe. Spika, sababu zinazopeleka meli kuzama wala haitegemei umri wa meli lakini ni sababu kubwa ambazo ni umakini na kutofuata maelekezo ya usafiri wa baharini. Naomba Mhe. Waziri hizi azikubali kuwa ni sababu za msingi.

Mhe. Spika, leo tunatengeneza sheria hii, sheria ambayo mimi ninaiita ni sheria ya kukopia. Ni hatari kubwa Mhe. Spika, kuwa na mwanafunzi anayependa kukopia. Mwanafunzi anayependa kukopia, ukimuandikia chochote yeye anaandika. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Waziri serikali hii na wananchi wa Zanzibar wanawalipa wataalamu wetu kwa ajili ya kazi, tusiwadharau kamwe wataalamu wetu kuwa hawana uwezo.

Mimi ninadhani bado wizara haijawakubali kuwatumia wataalamu wake na unawadumaza kwa makusudi kwa sababu ya nyenzo. Mhe. Spika, mimi naamini kwamba iwapo wataalamu wetu wa ZMA watawezeshwa kikamilifu wanaweza kutusaidia suala hili la usafiri wa baharini.

Lakini Mhe. Waziri nimuulize kwenye kitengo chake cha ZMA kuna *surveryors* wangapi, kama huna surveryors wa kuweza kuzikagua hizo meli utawezaje kuwa na sheria nzuri kwa ajili ya usafiri wa baharini. Leo hana surveryor na huyo aliopo mtaalamu pengine anamlipa shilingi laki tatu, lakini SUMATRA mtaalamu huyo analipwa shilingi milioni nne, ni tofauti kuwa na mtaalamu usiyemjali na mwenzako kuwa na mtaalamu akawa anamjali, ni tofauti kubwa sana.

Kwa hivyo kama tupo makini sana tuwezeshe wataalamu wetu na kitengo cha ZMA kiweze kufanya kazi. Kuliko kutoka miezi miwili mitatu kwenda kukopia sheria ya watu.

Mhe. Spika, mimi sipo radhi kusema kweli kuendelea kuwalipa wataalamu wetu fedha baadae ukawaambie *copy* and *paste*, ni aibu. Mhe. Spika, mimi sikubaliani kwamba kifungu cha kuongeza umri wa meli miaka 15 hakifai.
Sheria hii sheria mama kifungu cha 16 na 17 cha sheria mama kimeeleza wazi nini sifa ya meli kusajiliwa na wala sio ukongwe. Kifungu hicho hakikusema kabisa kwamba meli kongwe ndio haifai kusajiliwa, kimesema meli ambayo haina sifa kama zilivyoekwa kwenye sheria nazo ni

usalama wa abiria, usalama wa kimazingira na kufuata *regulations* za kimataifa. Hizo ndizo sifa na sio umri.

Leo anataka kuniambia MV Liemba miaka mia moja inafanya kazi kwa umri huo na SUMATRA hawa hawa ndio wanaoshughulikia. Leo waje wakwambie kwamba meli iwe na umri wa miaka 15. Kwa tafsiri hii maana yake meli ya serikali hivi sasa inatengenezwa kwa bilioni zaidi ya kumi na saba, maana yake baada ya miaka kumi na tano tuiangamize? Hii haiwezekani Mhe. Spika. Ni tatizo la umakini na kwamba wizara hii imeshindwa kusimamia wajibu wake.

Mhe. Spika, ikiwa mtu kashindwa wajibu wa kusimamia magendo ya tiketi, uje uweze kusimamia usalama wa baharini. Ikiwa tiketi zetu hapa zinauzwa kwa magendo kila siku, tiketi ya shilingi kumi na tano unauziwa kwa shilingi elfu arobaini, tupo tunaona hatushughuliki, uje useme sheria mbaya ni umakini tu hatujaamua.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninasema kwamba kifungu cha sheria hii hakina haja ya kurekebishwa, sheria mama imejitosheleza labda utwambie kuna mtu anahitaji aekewe tarehe hiyo. Kama kuna mtu ana meli yake mpya anahitaji kuileta ni sawa, tuambizane ukweli. Lakini sheria mama inatosha kuweka masharti ya usafiri wa baharini, mambo yote yameelezwa humu, wajibu wa msajili umeelezwa humu hamna dosari yoyote, tatizo tumeshindwa kusimamia.

Mhe. Spika, mimi kwa dhati kabisa siwalaumu wataalamu wetu hamuwashirikishi. Mtaalamu anadai vitendea kazi miaka kumi na mbili hajapatiwa, sababu fedha hakuna. Hivi leo ukiwaambiwa tupatie hiyo ofisi ya ZMA wamekodishwa pale Mlandege, nina hakika ukiingia mule basi hamna kitu.

Mtaalamu gani atabakia hapa. Tumekuwa tukizungumza hapa kuhusu kanuni za ZMA mwaka wa nne huu, wizara imeshindwa kupitia kanuni za ZMA lakini kwa sheria wameweza. Leo Mhe. Waziri anatwambia kuwa wamekaa na SUMATRA wiki mbili lakini kanuni za ZMA zimeshindikana.

Mhe. Spika, kule kwetu kulikuwa kuna mwanafunzi mmoja wa darasa la saba alikuwa mwalimu anamuuliza mbili na mbili ngapi, husema nne, ukimtishia kwa mkwaju husema sio nne ni saba. Kwa hivyo wizara hii Mhe. Spika, tusiwe na tabia ya kukopia.

Mimi ninawaambiwa Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu lazima Mhe. Waziri atwambie kuna nini, sababu ambazo zimeelezwa humu sio sababu za msingi hata kidogo kwa sababu meli yoyote huzama kongwe ikiwa kuna umakini na utaratibu hautofuatwa.

Mhe. Spika, kifungu cha 16 cha sheria mama kimeeleza sifa za kimataifa hasa kwamba msajili akiridhia kwa hali ya meli inayoomba kusajiliwa haiendani na usalama na inahatarisha uchafuzi wa mazingira, hiyo meli haitosajiliwa na hapa zimesajiliwa meli hizo, hata wataalamu wenyewe wanatwambia kwamba wanatoa maelekezo ya kitaalamu lakini kuna watu wanawaambia hiki wacha.

Mhe. Spika, hata ripoti ya Rais; Tume ya Rais ameiunda kwa ajili ya ile meli ya MV Spice imesema wazi kwamba inapendekeza umri wa meli angalau miaka 20. Tume-*spend a lot of*

*money* kwa tume ile Mhe. Waziri amekaa na SUMATRA anawaambia hii wacheni, tufuate hii yetu mpya. SUMATRA huyu huyu ndiye aliyefukuzwa hapa, mimi ningetegemea tulimfukuza kwa nini na leo munampenda kwa nini, mungetwambia basi tukajua.

Tumemfukuza kwa shangwe hapa kwamba hafai, leo ghafla kawa ni mtu mwema. Kwa hivyo basi mutwambie kwa nini alifukuzwa na dosari zipi na leo amekuwa na sifa zipi za kuletwa na sio kwa hili tu.

Mhe. Spika, mimi ninavyoamini kwamba mswada huu kama ule ambao ulikuja hapa kuhalalisha ma-*helmets* kwa shangwe tu, kumbe kuna mtu ana biashara yake anataka auze, hatuwezi kwenda katika nchi. Sio kama kuna mtu anataka kuuza biashara yake imemganda tufanye kazi, hatuwezi kwenda hivyo Mhe. Spika. Leo tumepitisha ma-*helmets* zogo mkamate mkamate, sasa hivi nani anayekamatwa? *Helmets* hakamatwi mtu, kufunga mkanda hakamatwi mtu, ni mashaka tu, kwa nini kuna mtu ana makontena ya *helmets* hajauza.

Mhe. Spika, serikali haiendi hivyo. Ni lazima uwe na sababu ya msingi kwa ajili ya maisha ya watu, tuache kumtungia mswada sheria mtu.

Mhe. Spika, wizara hii hii mwaka 2007 ilituletea *Public Private Parternership*, kwamba tushirikiane katika kuijenga nchi. Serikali tayari imeunda meli na kuna matajiri wawili au watatu kama Jaku wana meli, mimi nitashindwa kwa sheria hii na siwezi kutunga sheria kwa ajili ya watu wawili, lazima kila raia mwenye uhuru wa kufanya kazi afanye kazi.

Mimi nilikuwa na mpango na Mhe. Omar Ali Shehe kununua meli lakini kutokana na sheria hii itanishinda. Lazima nipate meli mpya na fedha sina na sikopeshwi; maana huyo anayekopeshwa ni mtu maalum na meli aendeshe mtu maalum na bandari afanye mtu maalum watu wengine wanyimwe.

Mhe. Spika, hivyo awe makini sana katika kujenga nchi, lazima tutoe uhuru kwa wananchi wote; Zanzibar wanataka kuekeza na serikali hii imetwambia wazi kwamba kipa umbele wapewe wazalendo. Mzalendo kwa kumtaka aje na meli mpya kama ya SMZ hatoweza. Cha msingi ni umakini, usimamizi na *commitment* ya serikali kuhakikisha kwamba sheria zinafuatwa. Sheria zipo ninatoa mfano huo kwamba sheria Nam.16 kuhusu sifa za meli zipo wapi kabisa, lakini kwa sababu watu hawafuati sheria arekebishe.

Hata miaka 15 itapitishwa baadae lebo yake itafutwa, watu watafanya tu kwa sababu sheria hawafuati. Mimi ninasema kama sheria hazifuatwi tuambieni kwa nini mumeshindwa kudhibiti magendo ya tiketi. Ni jambo dogo tu ni kumkamata mtu mukamtia ndani masaa manne mukamaliza hamuwezi. Leo munarukia SUMATRA, keshokutwa mutakwenda Kenya, Uganda ni mashaka tu.

Kwa hivyo *commitment* ndio muhimu, sio sheria kwamba ni mbaya hii. Mimi ninakwambieni kweli kuwa baada ya miaka 15 itakuja, keshokutwa mimi tajiri nitakwambia futa hii uweke miwili. Leo tunakwenda wapi, tunasukumana tu kwa matakwa ya watu fulani.

Hivi leo hapa tunapitisha sheria hapa ukimwambia Mhe. Waziri ZMA ipo wapi na inafanya kazi vipi, afisi ipo wapi, hakuna maelezo. Ninajua baadae atakuja kuniambia baada ya sheria hii ataandaa, utaandaa wapi, miaka kumi na mbili hatujamiliki kazi hii. Lengo ya sheria hii kwa kweli inanipa mashaka kwamba inaelekea kuwa kuna watu wana mitaji yao na biashara wanataka kufanya biashara isiyo halali.

Mhe. Spika, mswada huu kwa kipengele cha umri wa meli si kigezo cha kimataifa, si kigezo kwenye sheria mama na ni dhahiri kwamba Mhe. Waziri na wizara yake wana lengo ambalo hawataki kutwambia. Na ni vyema katika siasa za uwazi na demokrasi mutwambie kuna kwa sababu sheria hii mimi sioni dosari yake. Kifungu cha 16 na 17 kipo wazi juu ya usalama wa meli.

Mhe. Spika, eneo jengine tunaambiwa kila meli itabidi iweke vyumba viwili vya mafunzo ya baharia. Sheria hii pia imeeleza Mhe. Spika, wazi kuhusu mafunzo ya mabaharia.

Leo kuna boti ngapi hapa. Hizi boti tulizokuwa nazo ukivitoa hivyo vyumba viwili, maana yake si boti tena hiyo. Maana yake boti yenyewe vyumba viwili havitimii. Sidhani kama mimi Sea Bus ina vyumba viwili vya reserve au Kilimanjaro, kwa hivyo ukivitoa vyumba viwili maana yake hizo boti ndio ziondoke. Maana yake tunasukuma tu.

Sasa kama Sea Bus ziondoke, Kilimanjaro ni sawa na zitakuja meli mpya lakini ni dhahiri kwamba inaelekea kwamba hatupanuwi wigo wa kushindana kwenye usafiri wa baharini. Mhe. Spika, tukifika kwenye hatua hiyo lengo la nchi sasa ni kuipeleka katika ubepari, jambo ambalo si sahihi, si malengo ya mapinduzi matukufu ya 1964.

Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri sana kwamba aangalie wapi alipojikwaa sipo alipoangukia, ambapo tumejikwaa kutosimamia sheria zetu na sheria zipo. Mhe. Spika, ndio maana Mhe. Hamad akasema kwamba kuna haja ya Mhe. Abubakary huyu waziri wetu kuandaa sheria maalum za kuunguza au kuzitia moto sheria; maana zipo nzuri tu lakini hazifanyi kazi.

Hebu jaribu leo Mhe. Waziri utukamatie watu wawili wale wanaouza tiketi za magendo. Maana yake unawatafutia dawa kubwa, mtu awe na kitambulisho na kama huna huuziwi tiketi, watu pale pale wanauza tumeshuhudia. Sheria hiyo haisimamiwi tunaona na ukimwambia Waziri anakwambia maana yake hii ni biashara huria. Biashara huria hairuhusi kuuza magendo.

Mhe. Spika, mimi ninachosema kwamba suing mkono kifungu hiki cha miaka kumi na tano, sababu alizozitoa Mhe. Waziri ni dhaifu haziendani na sheria mama wala sheria za kimataifa, ni sababu ambazo kwa kweli tunataka kuilisha hasara taifa letu.

Mhe. Spika, mwisho sheria imesema mtu anaweza akasajili pahali popote. Hivyo Mhe. Spika, ni mfanyabiashara gani mwenye akili na pesa yake ataacha kusajili kwenye SUMATRA aje ZMA iliyokuwa haina ofisi, haina mwanasheria, haina watendaji wala kanuni, nani huyo. Nani mwenye fedha yake na meli yake atakayekuja hapa kusajili wakati kanuni hapana, mwanasheria hatoshi, bandari hapana. Maana yake ninashangaa.

Tajiri gari atakuwa na meli yake kuwa ya mabilioni aje asajili hapa. Kwa msingi huo serikali itakosa mapato, watu wote watakimbilia Bara. Mimi kama Mzanzibari sitounga mkono hilo. Munatafuta njia muwanufaishe SUMATRA na Tanzania Bara kwa ajili ya mapato ya usajili wa meli.

Mhe. Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate ufafanuzi. Ahsante sana.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mawili matatu katika mswada huu muhimu ambao umewasilishwa kwetu.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia hapa leo kwa pamoja kuendelea na shughuli zetu. Lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia vile vile.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utajikita katika kifungu cha 12, hapa kwenye marekebisho ya 17 (a). Mhe. Spika, mimi kidogo nimepata matatizo na mashaka kidogo kuona kwamba hapa tunasema hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka kumi na tano tokea tarehe ya kutumika kwake.

Nilifikiria labda ni lugha imekosea huenda nitakapoangalia huu msw

Nilifikiria labda ni lugha imekosea huenda nitakapoangalia huu mswada wa kiingereza nikaweza kupata usahihi wa neno lenyewe. Lakini nilipojaribu kuangalia huu mswada wa kiingereza nao vile vile unasema kwamba, "*No ship have no fifteen years of age from the date of commission, shall come for registration or licence for the purpose of carrying passengers Zanzibar".*

Hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie kinachokusudiwa hapa ni kutumika kwake au kuzaliwa kwa ile meli yenyewe, yaani kutengenezwa kwake. Hapo nilikuwa naomba ufafanuzi katika suala hili ambalo lipo hapa.

Halafu suala la pili nilikuwa vile vile naomba kueleweshwa kwa sababu humu nilipokuwa naangalia hapa makabrasha, nilikuta kuna maeneo kwamba madhumuni ya kuanzishwa kwa sheria hii ni kushirikiana baina ya Maritime Zanzibar na wale SUMATRA ambao wapo upande wa pili wa muungano. Sasa kule kuna sera na sheria ambazo wanazitumia na huku kutakuwa kuna sera, sijui kama itakuwa tayari zimekwishakutengenezwa au vipi na kuna sheria ambazo tutazitumia katika masuala haya.

Sasa hebu tusaideie namna ya uwiano na namna tutakavyoweza kuendesha hili zoezi letu kwa kutumia hizi sheria mbili ambazo mimi kwa upeo wangu naona zina tofauti kidogo katika utekelezaji wake.

Mimi nilikuwa ninataka kupata maelekezo ya vitu hivyo viwili tu. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, ninashukuru sana. Ahsante sana ninaunga mkono hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Aidha nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada huu wa sheria na pia niwapongeze wachangiaji mbali mbali waliotangulia katika kuuchangia mswada huu wa sheria. Michango yao ilikuwa inaelekeza katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo yetu ili kurekebisha sheria zetu, tuwe na sheria nzuri ambayo itasaidia katika kuhakikisha kwamba usalama wa wananchi wetu unakuwepo.

Mhe. Spika, sheria hii licha ya kuwa nia na dhamira yake ni kuhakikisha kwamba abiria wanaosafiri katika ukanda huu wa pwani yetu, wanasafiri wakiwa katika hali ya usalama wao na mali zao. Kuwepo utaratibu uliokuwa mzuri zaidi wa kuimarisha usafiri wa baharini ili uweze kufikia viwango stahiki vitakavyotuwezesha kufanya shughuli zetu hizi kwa usalama zaidi, hiyo ndio dhamira kubwa sana.

Mhe. Spika, tusisahau kwamba nchi yetu hii ilikumbwa na majanga makubwa ya kuzama kwa meli mbili katika kipindi cha karibuni na hasara yake kimaisha na kimali imetia manung'uniko na hasara kubwa kwa kukosa roho za wananchi wenzetu na mali kupotea. Kwa hivyo, serikali inapochukua jitihada ya kuhakikisha mambo kama yale hayatokei tena na kuweka utaratibu mzuri, mimi nafikiri Mhe. Spika, ni jambo la kuliunga mkono, ili tuwe na utaratibu mzuri zaidi utakaotuwezesha kuhakikisha usalama wa watu wetu na mali zao unakuwepo na hata kama ikitokea basi iwe ni kwa bahati mbaya sana.

Kizuri Mhe. Spika, katika Baraza hili, wakati yalipotokea yale Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili walikuwa wakali sana katika kuhakikisha kuboresha shughuli zetu ili ziendane na wakati. Leo tunaletewa sheria ambayo inaonesha njia ya kuhakikisha usalama wa watu wetu. Sio vibaya kukosoa na sio vibaya kushauri. Lakini tushauri katika ule msingi wa kujenga ambao utahakikisha usalama wa watu wetu. Haya yaliyofanywa na serikali hususan kuvitaka vyombo vyetu hivi viwili vishirikiane ZMA na SUMATRA. Nia ni kwamba vyombo hivi vifanye kazi kwa sura moja, mazingira yake Mhe. Spika, abiria wetu wasafiri kati ya Dar es Salaam na Zanzibar, Zanzibar na Pemba, Pemba na Tanga. Kwa hivyo, upande wowote ule utakaofanya makosa basi utasababisha upande mwengine kuingia katika hasara kubwa. Ni watu wetu hawa hawa wanaotoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam kibiashara, wanaotoka Dar es Salaam kuja Zanzibar kibiashara na shughuli nyengine za kijamii.

Kwa hivyo, ni lazima kuwepo na utaratibu wa mashirikiano utaohakikisha usalama wa kila upande, hata kama tutachukua hatua gani za kuhakikisha kwamba usalama unachukuliwa kwa upande wa Zanzibar tu na kama Dar es salaam kutakuwa na upenyu wa aina yoyote, basi matokeo yake tatizo litakuwepo pale pale. Kama wenzetu wa Dar es Salaam ndio watachukua hatua na Zanzibar hatukuchukua, basi matokeo yake tatizo litakuwepo pale pale. Lakini tunaposhirikiana, sio kuwa tunapeana kamandi, tunagawana uzoefu, tunashauriana kwa lengo moja la kuhakikisha watu wetu wanaosafiri katika bandari zetu hizi wako salama, maana ni ukanda huu huu. Kwa hivyo, ushirikiano wenyewe umekuja kwa ajili ya kutunusuru na kujifunza jema sio vibaya. Ukijifunza kwa Tanzania Bara, ukijifunza kwa Kenya, ukijifunza kwa Ulaya.

Mhe. Spika, ukiona liko jambo zuri ukajifunza basi litakusaidia katika kukuhakikishia shughuli zako zinakwenda vizuri Mhe. Spika, sioni ubaya wake. Kwa sababu nia yetu ni kutengeneza. Kwa hivyo, ushirikiano ni jambo zuri na ushirikiano huu Mhe. Spika, umekujaje. Ni baada ya

Baraza la Usalama la Taifa kukaa na kuona athari kubwa ya kupoteza maisha ya watu wetu, ilibidi Baraza liamuru kwamba vyombo hivi viwili vikiwa havikufanya kazi kwa pamoja vitaendelea kusababisha hasara kubwa kwa watu wetu na hasara yenyewe ni kupoteza maisha ya watu wetu. Mhe. Spika, ni lazima jitihada zichukuliwe ili kuonesha kwamba tunanusuru maisha ya watu wetu. Kwa hivyo, kila jema ambalo litasababisha kunusuru maisha ya watu wetu basi tulifanye. Lazima Mhe. Spika, tuwe wazalendo, tusifikirie kipato zaidi, tufikirie maisha ya watu wetu na sheria yetu hii Mhe. Spika, haimkatazi Mzanzibari au Mtanzania au mjasiriamali yeyote mwenye nia njema ya kufanya shughuli zake kwa kufuata vigezo vitakavyohakikisha usalama wa watu wetu. Hata uwe na uzalendo gani, kama utasababisha kupoteza maisha ya mwenzako uzalendo huo uko wapi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ninachozungumzia hapa ni usalama wa watu wetu, hatuwezi tukaweka tamaa mbele tukaona watu wetu wanakufa tukanyamaza kimya. Kwa hivyo, msisitizo wake hapa ni uzalendo wetu kwanza uone uhai wa watu wetu. Hatukatazi mtu yeyote Mhe. Spika, na serikali yetu kila siku inajenga mazingira mazuri ya *private sector*, kufanya wajibu wake vizuri. Ndio maana tumefikia hatua ya kuwa na Baraza letu la Biashara na iko ile *private and Public Partnership*. Tunakaa pamoja kutafuta kila aina ya wafanyabiashara wetu watakavyoweza kufanya biashara zao vizuri zaidi. Kwa hivyo, mazingira tunayoyajenga ni kwamba wafanyabiashara wetu wafanye, lakini kwenye jambo la uhai wa watu wetu ni lazima tulifanye kwa kuhakikisha usalama wao upo, inapotokezea bahati mbaya basi iwe bahati mbaya.

Mhe. Spika, umetoka ushauri mzuri hapa kwamba kama uwezo wa watu wetu ni mdogo kwa mtu mmoja kuweza kununua chombo kizuri kitakachokidhi vigezo, kwa nini tusishirikiane tukawa wengi zaidi ili tukanunua chombo kizuri, kikafanya kazi vizuri na usalama wa watu wetu ukapatikana. Ni kujenga tu mazingira ya kufanya kazi kwa pamoja na kuaminiana tukajirekebisha penye kasoro popote. Lakini Mhe. Spika, asili ya mswada kuja hapa ni kupata maoni na ushauri wa Wajumbe. Mara nyingi kama serikali tunapopata ushauri sahihi hatuwezi kukataa Mhe. Spika, tunafuata yale ambayo tunaambiwa. Sasa sisi kigezo chetu cha kuja na umri wa miaka 15 ni jambo ambalo tulishauriwa kitaalamu kabisa na tukaona umuhimu kwamba miaka 15 ndio umri mzuri utakaowezesha vyombo vyetu kufanya usafiri vizuri. Sasa hapa kama Waheshimiwa Wajumbe wataona kuongeza kwa umri wakaleta hoja vizuri na kuhakikisha kwamba vyombo hivyo vitakavyokuwa na umri wa zaidi ya miaka 15 vitakuwa madhubuti na usalama wa watu wetu na wao wakachukua *assurance* hiyo basi wananchi watawasikia, waseme hivyo waeleze Mhe. Spika.

Kwa hivyo, hatuji hapa kulumbana, tunakuja hapa kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha maslahi ya watu wetu na uhai wao, sheria hii inagusa maisha ya watu wetu. Nilikuwa naomba Mhe. Spika, katika michango yetu tujielekeze kuwa na sheria nzuri itakayotuhakikishia usalama wa watu wetu, itakayohakikisha kwamba shughuli za usafiri wa baharini zinafanyika vizuri na zinawavutia wageni wetu kuja. Tunapokuwa na vyombo ambavyo havikidhi viwango, hata sekta yetu kubwa ya utalii basi itaporomoka Mhe. Spika. Watu walikuwa wanaanza kuogopa sasa kuja Zanzibar kwa sababu wanaona kuna vyombo vibovu. Kwa hivyo, sekta yetu tunaitumainia ituendeshee maisha yetu sana. Tunapofanya marekebisho ya mambo haya, huwa tunaangalia kwenye maeneo mengi kwa nia ile ile ya dhamira ya kuimarisha uchumi wetu na dhamira ya kupambana na umaskini ili tuwe na maisha yaliyo bora zaidi. Kwa hivyo, mimi nawaomba Waheshimiwa tuchangie mswada wetu huu ukielekeza umuhimu wa kujali maisha ya watu wetu,

ukielekeza umuhimu wa kuwa na sheria nzuri itakayotusaidia kwa maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nikaweza kutoa mawili au matatu katika sheria hii.

Mhe. Spika, pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kutuletea mswada huu mzuri ambao kama walivyozungumza waliopita kwamba hata ulitokana na matatizo mengi ambayo yaliyojitokeza katika kipindi hiki cha karibuni kutokana na maafa mbali mbali yaliyotokezea kwa wasafiri katika eneo la baharini.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka niseme kwamba huu mswada sio mbaya, mswada ni mzuri na kimsingi kama alivyomaliza hapa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tuweze kutoa maoni ambayo yataweza kumsaidia Mhe. Waziri ili hii sheria sasa hivi ikawatumikie wananchi wetu.

Mimi nataka nianze kwa kusema, kama kawaida yangu kwamba Zanzibar katika nchi ambayo inaongoza kwa sheria nyingi nzuri basi sisi Zanzibar nadhani hatufiki hata wa tatu katika Afrika, kama sio wa kwanza basi hatufiki nchi ya tatu, lakini tatizo linarudi pale pale Mhe. Spika, kwamba tatizo letu linakuja katika utekelezaji na usimamizi wa zile sheria ambazo tunazitunga. Sasa mimi ninaamini hii sheria tuliyokuwanayo wala ilikuwa sio mbaya, ilikuwa ni nzuri sana, lakini tulikuwa na tatizo lile lile la kawaida la kutosimamia vizuri majukumu yetu. Kwa hivyo, ninaamini pamoja na mapungufu yaliyotokea na marekebisho haya tutakayoyafanya leo, basi naamini Mhe. Spika, tutaweza kuwatendea sana haki wananchi wetu kwa kuwatengenezea sheria nzuri ambayo itakayoweza kuwalinda pamoja na sisi wenyewe kwa usalama wa maisha yao.

Mhe. Spika, mimi namuomba sana Mhe. Waziri awe msimamizi wa karibu sana na awe mkali sana katika kusimamia hizi sheria ambazo tunazipitisha. Ninaamini kwa ninavyomjua Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri wake, wataweza kushirikiana kwa karibu katika kusimamia sheria ambazo tunazipitisha. Kwa sababu Mhe. Spika, wizara hii tumewapa mzigo mkubwa sana, tumewapa malango makuu ya uchumi katika nchi yetu yako chini ya usimamizi wao. Sasa kutosimamia vizuri basi kuna hatari kubwa hata kuathiri uchumi wa nchi yetu.

Kwa hivyo, kitu ambacho nakiomba Mhe. Waziri na yeye kwa bahati nzuri alikuwa sio mkosoaji, lakini alikuwa ni mwelekezaji mkubwa kwa serikali katika mambo mbali mbali, kwa hivyo naamini umahiri wake huu na huko aliko ataweza kuutekeleza vizuri.

Mhe. Spika, nataka nije kidogo niguse mawili au matatu katika sheria hii. Mhe. Spika, katika sheria hii au katika mswada huu ambao baadae tukishaupitisha utakuwa sheria, unasomeka kwa jina fupi inasema, sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini ya mwaka 2012 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais.

Mhe. Spika, mimi hapa nilikuwa nataka nije kupata maelezo kidogo. Tunajua kuwa mswada huu uliandaliwa tokea mwaka 2012, lakini leo tuko mwaka 2013. Sasa nilikuwa nataka tu ufafanuzi kwamba hili jina fupi baada ya kupitisha mswada huu, napendekeza iwe marekebisho ya sheria

ya usafiri wa baharini ya mwaka 2013. Kwa sababu tukisema mwaka 2012 ina maana mswada huu tuliupitisha mwaka jana. Sasa hapa tu kidogo nilitaka nije niwekewe sawa.

Jengine Mhe. Spika, kwa kuwa sheria hii kifungu cha pili kinasema sheria hii itasomwa pamoja na sheria ya usafiri wa baharini nambari 5 ya mwaka 2006, ambapo katika sheria hii itajulikana kama ni sheria mama. Sasa huku mbele katika kifungu cha 6 cha sheria hii nilikuwa kidogo nataka nipate ufafanuzi, kwa sababu kifungu cha 6 kinasema kifungu cha 7 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (2) neno "Tanzanian" na badala yake kuweko neno "Tanzania".

Lakini kifungu kidogo cha (2) kinasema kubadilisha maneno "Zanzibar Tanzania" yanayojitokeza baada ya maneno "usajili wa" na badala yake kuweka neno "Zanzibar". Marekebisho hayo yatatumika kila sehemu ambapo maneno "Zanzibar Tanzania" yamejitokeza. Suala hili mimi nalipongeza kwa sababu ni kweli katika sheria ile lugha hii kidogo ilikuwa inachanganya, kwa sababu Zanzibar ni Zanzibar.

Lakini Mhe. Spika, kitu ambacho nilikuwa nakitaka zaidi ufafanuzi wake ni hapa kwenye kifungu cha 5(6)(3) ambacho kinarekebishwa kwa kufuta maneno "chombo cha usimamizi wa usalama wa baharini kilichoanzishwa chini ya sheria ya usafiri wa baharini ya mwaka 2003" na badala yake kuweka neno "*SUMATRA*" kama ilivyoanzishwa chini ya sheria ya mamlaka ya kusimamia usafiri baharini ya mwaka 2001, kama inavyobadilika kila baada ya muda.

Mhe. Spika, eneo hili hata Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amelizungumza. Lakini mimi nilikuwa nina khofu moja, hapa Mhe. Spika, tunatunga sheria na kwa kuwa tunatunga sheria, naomba tusitengeneze kitu ambacho kinaweza kikakwaza utendaji wa shughuli wa hii sheria ambayo tunaitunga.

Mhe. Spika, mimi ninavyojua *SUMATRA* ni chombo ambacho kinachosimamia masuala ya usafiri kwa upande wa Tanzania Bara, na sisi sheria tunayoitunga sio sheria ya Muungano, hii sheria ni ya Zanzibar moja kwa moja. Sasa tunapokitaja chombo moja kwa moja, hapa itakuwa Mhe. Waziri kama mfano chombo hiki tulichokitaja hatukutekeleza majukumu yake kikamilifu, Mhe. Waziri huyu sijui atakuwa na mamlaka gani ya kuweza kukiwajibisha kile chombo chengine. Kwa hivyo, tunapotunga sheria naomba tutunge sheria inayojitegemea, tusitunge sheria ambayo tunaingiza kitu ambacho Mhe. Waziri moja kwa moja hana mamlaka nacho.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba kwamba ni vyema mamlaka ya usafiri wa baharini ya Zanzibar, mimi nadhani tunaweza kuweka kwamba katika uhakiki wa meli au usajili wa meli katika ukaguzi, basi iwe inaweza kushirikiana na chombo chengine chochote ambacho chenye mamlaka kama wao. Sasa hapo moja kwa moja umeshaipa mamlaka mpaka ya kushauriana na wenzao wa *SUMATRA*, kuliko kukitaja moja kwa moja tukakiweka kwenye sheria.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya wenzangu wamesema kule wenzetu katika ule uundwaji wa *SUMATRA* kuna sera na sheria. *SUMATRA* haishughulikii tu masuala ya usafiri wa baharini, lakini ni mpaka usafiri wa nchi kavu vile vile. Sasa tusije kufika pahala ikawa tena mamlaka ya usafiri wa nchi kavu tukaja tukaanza tena na *SUMATRA* watie mkono wao. Sina madhumuni ya kukataa ushirikiano, hakuna kitu kizuri duniani kama ushirikiano, lakini tunapotunga sheria kuna

baadhi ya mambo lazima tuweze kuyaweka wazi kabisa ili tusijifunge moja kwa moja. Kwa sababu sisi meli zetu zinatembea mpaka mwambao wa Mombasa vile vile. Kwa hivyo, wakati mwengine tunaweza kushirikiana na chombo ambacho pengine kinachotumika nchini Kenya kwa ajili ya kuweza kuimarisha hizi shughuli zetu. Sasa hapa ndio maana nikasema kwamba tunapoweka moja kwa moja chombo tukakitaja, ina maana tunajifunga sasa kukialika chombo chengine kuja kushirikiana na mamlaka yetu ya usafiri wa baharini katika kuboresha zile shughuli zake.

Kwa hivyo, mimi napenda tuwe na mashirikiano mazuri, lakini mamlaka ile sasa hivi tuipe uwanja mpana wa kuweza kushirikiana au kushauriana na mamlaka nyengine yoyote tusiitaje moja kwa moja kwenye sheria, kwa sababu hapo baadae inaweza ikatuletea matatizo.

Mhe. Spika, nikiendelea nakuja katika kifungu cha 10(a) cha sheria hii. Samahani kidogo Mhe. Spika, unajua utuuzima unakuja, macho haya ndio hivyo tena. Mhe. Spika, kifungu chenyewe nakusudia kinachozungumzia suala la faini. Kifungu cha 10(a) (2) kinasema;

Kifungu cha 10(a) (2)

> "Mtu yeyote atakayevunja masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kijifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na atahukumiwa kwa kulipa faini kiasi kisichopungua dola 5,000".

Sasa Mhe. Spika, najua katika nchi yetu hapa tunatumia Tanzania shillings, ingawa kuna baadhi ya kodi zetu tumeziruhusu kulipiwa kwa dola. Lakini hapa linapokuja suala la kifungu hiki unaposema, mtu anatakiwa alipe faini ya kiasi kisichopungua dola 5,000. Mimi nadhani tungeongeza na maneno au shilingi za Tanzania, au *equivalent* kwa shilingi za Tanzania. Kwa sababu ina maana tukiweka dola tu moja kwa moja, ina maana tunaishusha thamani pesa yetu ya Tanzania.

Mhe. Spika, kuna siku moja nilimsikia Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akasema kuna baadhi ya nchi za wenzetu, sijui kama Zimbabwe au nchi gani, ile kwenda dukani au kwenda katika taasisi yoyote kutumia pesa ambayo sio ya nchi ile basi ni kosa kubwa sana kisheria. Akazungumzia kutumia tu dola kuruhusu matumizi ya dola kila pahala, wakati mwengine hata ule uimara wa fedha yenu ya nchi mnakuwa mnauregezaregeza. Ile mamlaka ambayo ina-*regulate* ile thamani ya pesa mnakuwa mnaipa mashaka makubwa sana, kwa sababu watu wengine wanatumia *loop hole* ile ile ya kwamba baada ya kutumia matumizi ya Tanzania shillings wanatumia dola, halafu baadae mule mule wanapata kufanya udanganyifu. Sasa ili kuendelea kuipa heshima na nguvu pesa yetu ya Tanzania, mimi nadhani tungeweza kuongeza maneno au sijui kwenye marekebisho labda kwenye Kamati, kwa sababu Mhe. Spika, kama nilivyokuandikia kidogo nilikuwa kwenye safari, sikuweza kukaa vizuri na kujiandaa. Nadhani kama hayo hayakuonekana, basi nilikuwa naomba kwamba katika kifungu hiki, basi ingeongezwa matumizi ya pesa ya Tanzania. Kama imefanywa hivyo kwenye Kamati basi naungana nao mkono moja kwa moja.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika kifungu chenye maneno, yaani kifungu cha 17. Kama nilivyokuambia Mhe. Spika, macho yangu haya halafu kutokana na misafara sikuweza kujiwekaweka vizuri sana, miwani waliyonipa hailingani na macho yangu.

Kifungu cha 17(a) (1)

> "Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake, itakayosajiliwa au kupewa usajili wa kuchukua abiria na mizigo hapa Zanzibar".

Mhe. Spika, na ukiona jambo limesemwa basi ujue kuna jambo. Mimi nataka kama alivyozungumza Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hii sheria ndio imekuja kwetu ili tuweze kutoa maoni. Mhe. Spika, Kamati imekaa na wadau. Tena nakupongeza sana Mhe. Spika, utaratibu ambao umetuanzishia sasa hivi ni utaratibu mzuri sana na utaratibu huu unapata nafasi ya wale wadau au wahusika wa ile sheria wanaoitumia moja kwa moja kuweza na wao kutoa maoni yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani na wala sikuwemo kwenye Kamati, lakini naamini wadau hili ni suala ambalo walilizungumza sana.

Vile vile nataka nimpongeze sana Mhe. Rais kwa ile Tume aliyoiunda kwa ajili ya kushughulikia hizi ajali za meli na kama sikosei kwa sababu hii tume ya mara ya pili sikupata kuikaribia zaidi, isipokuwa nilisoma zaidi yale mapendekezo yao ya ile tume ya mwanzo.

Kwa kweli Tume ile ilikuwa ni makini sana Mhe. Spika, na nadhani Mhe. Rais akairejeshea tena na sijui kama kuna Wajumbe walipungua au waliongezeka akairejeshea tena kuunda ya MV. Skagit. Mhe. Spika, tume ile imefanya kazi kwa uadilifu mkubwa sana na tunawapongeza.

Kwa hivyo, naomba sana kama heshima aliyoitoa Mhe. Rais kwa Tume ile basi na mimi nataka tume ile niipe baraka kwa kuweza kusisitiza yale maoni waliyoyatoa katika mapendekezo ya hizi Sheria za Usajili wa Meli. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani kwa meli kwamba tokea tarehe iliyoanza safari kwa miaka 15 kwa kiasi fulani tutakuwa tunajibana sana, nafikiri tungeliweka miaka 20, kwa sababu hata ile tume ambayo ilifanya kazi kubwa ya kufanya utafiti wa nchi mbali mbali duniani na kuangalia mazingira ya nchi husika.

Mhe. Spika, nafikiri Mhe. Waziri atukubalie na iwe angalau miaka 20, kwa sababu mambo haya Mhe. Spika, ni *nipe nikupe* kwa sababu Mhe. Waziri ameleta mswada na tunautia nyama na sisi tunaomba miaka 20 sio mingi.

Mhe. Spika, nataka nimueleze kitu kimoja Mhe. Waziri nadhani Mhe. Spika utakubaliana na mimi, kwamba chuma cha zamani na kile cha sasa ni tafauti. Kwa kweli naamini chuma cha zamani umadhubuti wake, Mhe. Spika inaonesha Waheshimiwa Wajumbe hawajanielewa. *(Kicheko/Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, chuma kwa maana ya *iron*. Chuma cha kutengenezea meli ndicho anachozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma. *(Kicheko/Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, nakusudia kile chuma cha pua kinachotengenezewa meli. Sasa uimara wa chuma cha zamani huwezi ukaulinganisha na uimara wa chuma cha sasa.

Kwa hiyo, hata Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anakubaliana na mimi kwa sababu naona ametikisa kichwa. *(Kicheko/Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikatoa mapendekezo yangu nikasema basi kwa meli iliyotengenezwa miaka 20 iliyopita naamini bado chuma chake kiko madhubuti na kikipata kutu kidogo kinakuwa hakitetereki tofauti na vyuma vya hivi sasa kikipata kutu kidogo basi unakikuta tayari kimeanza kupinda. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani kwa umri wa meli miaka 20 sio tatizo kuweka kwenye sheria yetu. Kwa hiyo, nafikiri suala hili wala tusifike pahala tukampa tabu Mhe. Waziri katika vifungu, kwa sababu mimi nadhani ameleta mswada huu kwa ajili ya *negotiation*, tena nafikiri suala hili yeye mwenyewe Mhe. Waziri atakuwa anakubaliana nalo.

Mhe. Spika, naomba kurejea tena isipokuwa usimamizi hasa wa hizi mamlaka ambazo tunazozitungia sheria. Kwa mfano, wenzangu wamezungumza na hata na mimi nilisikia ile meli ilioko kule kwenye ziwa *Victoria* kama sikosei naambiwa ina umri karibu miaka 100 sasa ule ndio uimara wa chuma niliouzungumza pale mwanzo.

Sasa kitu kikubwa ambacho nadhani na pia tuweke masharti na nafikiri kwenye hii sheria huko mbele nadhani imo, kwamba zile *regular maintenance* zile ndio muhimu, kwa sababu zinapelekea kwamba wale wakaguzi wa vyombo kila wakati wanapata kukiangalia uimara wake pamoja na ubora wake, na kama kwenye marekebisho waweze kutoa hayo marekebisho.

Kwa hiyo, nadhani tukiweza kulifanya hilo, basi nafikiri wawekezaji wetu ambao ni wazalendo kwa hali zao tunazijua na wamesaidia sana kwenye usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, matatizo yaliyojitokeza mimi nataka niseme ni uzembe tu wa kibinadamu, kwa sababu mara nyingi hizi ajali zilivyotokezea hazikusababishwa hasa na umri, isipokuwa zimesababishwa hasa na ile *capacity*, kwamba ule uwezo wa kubeba abiria ulikuwa maradufu zaidi.

Kwa mfano, hata gari Mhe. Spika sisi tunazo gari ikiwa gari yako mwenyewe ukiipakia mzigo ukizidi kidogo tu basi unahisi wakati unapopiga *cross* unahisi inakuvuta tofauti na ile hali ya kawaida.

Kwa hivyo, nadhani vyombo vyetu hivi vikiweza kusimamia vizuri hizi kazi zao tulizowakabidhi, basi naamini itakuwa hakuna mashaka. Kwa maana hiyo, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa sheria hii.

Vile vile kifungu cha 17(a) (1) (3) Mhe. Spika naomba kidogo nikinukuu.

Kifungu cha 17(a) (1) (3) cha mswada kinaeleza hivi:-

> ‘Hakuna meli itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa madhumuni ya kuchukua abiria ndani ya Zanzibar ikiwa meli hiyo imebadilishwa kutoka katika asili ya utengenezaji wake, kwa madhumuni ya kijifungu hichi mabadiliko inasema,

maana yake ni mabadiliko yoyote yatakayobadili muundo wa meli, hili nakubaliana nalo katika uhalisia wake kama vile ukubwa, nakubaliana nalo, upana nakubaliana nalo, kina cha kufungia hili sina utaalamu nalo sana, lakini mashine za umeme na vyombo vya mawasiliano au vinavyofanana na hivi'.

Mhe. Spika, mimi naomba nije kwenye mashine za umeme. Kwa kweli kama tunavyojua chombo chochote ambacho kitakachokuwa kinakaguliwa, basi lazima kuna kipindi wale wakaguzi watawaambia, kwamba aidha hii *engine* uwezo wake umepungua au umemalizika na tunataka utafute *engine* nyengine au kifaa chengine kilichozungumzwa kwamba mashine ya umeme, yaani ile mashine ya kuzalishia umeme kama ukiacha *engine* kuna chombo chengine, basi bila ya shaka nacho kitafika pahala kitatakiwa kitolewe kiwekwe chengine.

Sasa unaposema mabadiliko mpaka kwenye mashine za umeme au vyombo vya mawasiliano hapa kidogo mimi nitapata mashaka, kwa sababu meli nyingi tutafika pahala tutaziacha zisifanye kazi yake wakati bado zinao uwezo wa kufanya kazi kutokana na vyombo hivi vya kuzalisha umeme.

Kwa kweli chombo cha kuzalisha umeme wale wakaguzi wakishasema kwamba umeme unaozalishwa ndani ya chombo chako pengine haufiki *voltage* fulani na hauwezi kuvuta mashine ya aina fulani na badala yake tunataka uweke chombo ambacho kitaendana nacho.

Mhe. Spika, mimi nadhani haya ndiyo *regular maintenance* yenyewe, vyenginevyo itakuwa hakuna haja ya kuweka ile Mamlaka ya Ukaguzi.

Nafikiri katika haya marekebisho kwenye mashine za umeme, vyombo vya mawasiliano na hata hii winji, kwa sababu wakati mwengine winji inakufa nguvu. Mhe. Spika, winji ikifanya kazi sana basi baadaye inapungua nguvu, sasa winji ikipungua nguvu haiwezi kubeba mzigo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, winji ikiwa haiwezi kubeba mzigo basi lazima itahitaji kufanywa ukarabati na iweze kubeba mzigo. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anatikisa kichwa, kwa sababu yeye ni mtaalamu sana na analijua hilo. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, hata winji inapofika pahala wale wakaguzi wameshasema winji hii haiwezi kubeba mzigo wa tani fulani, basi nadhani kuwe na uwezo wa kuweza kufanya marekebisho ya winji au *engine* hiyo.
Kwa hivyo, hili kidogo Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kutoa ufafanuzi pengine kuna mambo muliyarekebisha mimi sikuyaelewa, basi naamini atakuja kunipa ufafanuzi na kuelewa zaidi.

Mhe. Spika, kifungu cha 18(a). Kifungu hichi cha sheria hii kinaweka hapa kanuni na naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika.

Kifungu cha 18(a) kinaeleza hivi:-

> “Waziri anaweza kutunga kanuni zitakazoeleza ukomo wa umri wa meli zisizokuwa za abiria kusajiliwa kupewa leseni Zanzibar”.

Mhe. Spika, hapa tunalo tatizo na kwa nini hapa nikasema kuna tatizo. Kwa kweli tatizo kubwa linalotukabili katika nchi yetu ni kutunga kanuni na hizi sheria tukishazipitisha, yaani ukishampa mamlaka waziri kutunga kanuni, ina maana kama atachelewa hajatunga kanuni, kwa hiyo ule utekelezaji wa sheria ile Mhe. Spika unakuwa na ugumu wake.

Kutokana na hali hiyo, nadhani Mhe. Spika labda hapa Mhe. Waziri tumlazimishe, maana yake hapa inasema Mhe. Waziri anaweza kutunga kanuni, yaani akitaka anaweza. Kwa hivyo, sisi tukija hapa siku moja likatokezea tatizo na Waziri ikawa hajatunga kanuni na tukija kumsomea kifungu hichi atasema aa! Anaweza.

Kwa hiyo, nadhani tungelisema kwamba Waziri atalazimika kutunga kanuni, nafikiri tukisema atalazimika kutunga kanuni, basi waziri baada ya kupitisha sheria hii lazima akimaliza tu ataanza kuwaagiza watendaji wake tayari waanze kumtengenezea kanuni, kwa sababu anajua ile sheria imemlazimisha, lakini kwa hivi tunavyoiweka.

Mhe. Spika, zipo sheria hapa tayari tumeshazitunga na nyengine zinaweza kufika zaidi ya miaka mitano na kanuni hakuna na sheria haiwezi kumaliza kila kitu. Sasa wakati mwengine katika ile sheria kama haikuweka kanuni, kwa sababu kanuni ndio muongozo zaidi wa kuweza kufafanua utekelezaji wa ile sheria kwenye utekelezaji wa mambo madogo madogo pengine hata mambo ya ushirikiano.

Kwa kweli nadhani na hata lile nililolisema mwanzo la kushirikiana na wizara na hii hata kwenye kanuni linaweza kuwekwa. Kwa hiyo, na sheria hii tunavyoitunga nadhani kanuni ni muhimu sana na namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika ajitahidi basi angalau wamechelewa ndani ya miezi sita akiweza kututungia kanuni, na kwa sababu mimi najua kwenye wizara yake kuna wataalamu wengi ambao waliobobea, basi naamini suala hili ataweza kuliharakisha, ili sheria yetu hii iweze kufanya kazi vizuri na kusiwe na matatizo yoyote.

Mhe. Spika, mswada huu kama nilivyosema kwamba sheria hii ndio ngeni ambayo ni ya zamani, na kama tutakuwa makini katika kusimamia yale maamuzi yetu, basi naamini Mhe. Waziri ataweza kufanya kazi kwa vizuri, vile vile na wananchi wetu wataweza kufaidika na huduma wanayoipata.

Sasa la mwisho kabisa Mhe. Spika nataka niwapongeze sana wenye vyombo vya usafiri wa baharini hivi sasa. Mhe. Spika, sisi tumekuwa tukisafiri mara kwa mara kwa usafiri wa baharini na zaidi baada ya kuzifanya kuwa nzuri zaidi hivi sasa.

Mhe. Spika, nafikiri tulipitisha mpaka sheria kama sikosei na ikiwa hatujapitisha sina hakika vizuri, lakini wakati wa bajeti tulizungumza sana, kwamba wasafiri hivi sasa lazima waweze kutumia vitambulisho, ili kuweza kuondoa utata na matatizo wakati yanapotokezea majanga ya aina mbali mbali.

Suala hili lilizungumzwa kwa muda mrefu, lakini hivi sasa tunashukuru sana linatekelezwa kwa vitendo. Kwa mfano, hivi sasa kuna kampuni kama hujenda na kitambulisho basi tiketi huwezi kupata na wenzetu kule Tanzania Bara wao naona wamekuwa makini zaidi hata kama ukiwa na tiketi basi lazima uoneshe kitambulisho chako pale getini.

Jambo hili Mhe. Spika, linatusaidia hata kuzungumza yale ambayo tulikuwa tukiyazungumza kipindi cha nyuma kwamba Zanzibar watu wamekuwa wanaingia bila ya utaratibu, hii nafikiri imeweza kutusaidia sana.

Ingawa tayari kuna baadhi ya mapapasi tumeanza kuwaona na tiketi mkononi. Mhe. Waziri naomba kupitia kwako Mhe. Spika, isiwe kila siku tunakuja hapa kwa ajili ya kuwasakama tu, isipokuwa tunataka wakati tunapokuja kutoa maelekezo pamoja na kuwapongeza kwa ile jitihada wanazozifanya.

Kwa hiyo, tunaomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba awaagize watendaji wake watamuangusha, kwa sababu sisi tunajua Mhe. Waziri hakai pale chini ya Mkungu na kuangalia pale nani anayeuza tiketi mkononi, lakini kuna vyombo hivi ambavyo tunavyovipitisha kwenye sheria ndivyo tunavyovipa mamlaka ya kuweza kusimamia yale tunayoyazungumza hapa.

Mhe. Spika, sisi hatutaki kuona au kuonekana kama labda hapa tunawasakama mawaziri fulani hakuna, isipokuwa sisi kila atakayeshindwa kuwasimamia watendaji wake sisi huyo ndiye chakula chetu! *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, ambaye ni swahibu wetu tusije tukafika huko, kwa kweli pale bandarini tayari tumeshaanza kuona watu wanazo tiketi mikononi wanauza, wanazipata wapi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, usije ukaona yanatokezea yaliyotokezea na sisi kitu ambacho hatukipendi sana, na kwa sababu hivi sasa hata ukiingia katika meli unajihisi uko katika hali ya utulivu, yaani umeingia kwa mujibu wa idadi ya kile chombo kinavyohitajika. *(Makofi)*

Kwa kweli nawapongeza sana wenye vyombo vya usafiri wa baharini, lakini isiwe kama yale maneno ya mgema akasifiwa na tembo akalitia maji. Kwa hivyo, tunaomba waendelee kutusaidia kuchunga maisha yetu wakati tukiwa katika usafiri wa baharini. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura naunga mkono hoja hasa baada ya Mhe. Waziri baada ya kukubali yale mapendekezo ambayo wengi wameanza kuyapendekeza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu *Azza Wajalla* kwa kutujaalia neema zake, na kuendelea kukutana hapa tukiwa hai na wazima kujadili masuala yanayohusu nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia machache kuhusiana na Mswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri wa Baharini Nam. 5 mwaka 2006.

Tatu Mhe. Spika, naomba nimpongeze *back bencher* wa zamani Mhe. Waziri mpya na bado namwambia mpya wa Miundombinu na Mawasiliano Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa kuleta mswada huu hapa Barazani.

Mhe. Spika, nikiangalia maudhui ya marekebisho yaliyoletwa hapa ya mswada huu, inaondosha wasi wasi kwamba lengo lake ni kutekeleza sehemu ya mapendekezo ya Ripoti za Uchunguzi wa Ajali Mbili za Meli ambazo zimetokea Zanzibar katika kipindi cha karibuni, yaani ajali ya Meli ya MV. *Spice Islanders* na MV. *Skagit*.

Kwa kweli hili ni jambo la kupongezwa Mhe. Spika, kwamba serikali imepokea mapendekezo na kuamua kuyafanyia kazi. Kwa hivyo, tunapongeza hatua hiyo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Lakini nitakuja kwenye baadhi ya vifungu vya mswada ambavyo nataka kuvitolea maoni.

Vile vile naomba niungane na wenzangu ambao waliochangia hapa na kuonesha wasi wasi kwamba inaonekana ni kama vile tunadhani kufanya marekebisho ya sheria pekee ndio kunakoweza kurekebisha yale matatizo makubwa yaliyopelekea vifo vya wananchi wetu zaidi ya 2000 Mhe. Spika.

Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura leo amerejea maneno yake ambayo anapenda kuyasema humu ndani, kwamba kwa sheria tu pengine Zanzibar tunaongoza sana katika nchi nyingi kwa kuwa na sheria nyingi tena nzuri, lakini suala kubwa linakuja katika usimamizi au utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Spika, yako mambo ambayo nimeyaona kwenye mswada huu ambayo ni mazuri, lakini yako mambo ambayo yananipa wasi wasi na nitamuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie maelezo.

Mhe. Spika, yale ya jumla nitayaweka mwisho kwanza naomba niende kwenye mswada. Kwanza naomba nikizungumzie kifungu cha 5 cha mswada huu. Mhe. Spika, kifungu hichi kinarekebisha kifungu cha 6(3) (a) cha sheria mama Mhe. Spika, naomba kunukuu.

Kifungu cha 6(3) (a) kinaeleza hivi

> "Ambapo imesema inarekebishwa kwa kufuta maneno chombo cha usimamizi wa usalama baharini kilichoanzishwa chini ya sheria ya Usafiri wa Baharini 2003 na badala yake kuweka neno *SUMATRA* kama ilivyoanzishwa chini cha Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Usafiri wa Baharini 2001 kama inavyobadilika kila baada ya muda".

Mhe. Spika, na mimi niungane na wenzangu kusema kwamba marekebisho haya yanayotaja kwa jina *SUMATRA* mimi siyaungi mkono, Mhe. Spika kwa nini nasema hivyo, ukitizama sheria hii ambayo ndiyo inarekebishwa hii imeitambua mamlaka ambayo inasimamia usafiri baharini kwa

upande wa Tanzania Bara na kutaka kushirikiana, lakini haikutaja *SUMATRA*. Kwa hivyo, mimi sioni kwa kutaja *SUMATRA* tunaongeza chochote katika kuongeza ufanisi wa usimamizi wa usafiri baharini.

Kwa maana hiyo, kama lengo letu ni kuongeza ufanisi kwa kutaja *SUMATRA* bado hujataja kitu Mhe. Spika na ni jambo la kawaida kwa watunga sheria, kwamba mara nyingi unataja jina la jumla la chombo kinachosimamia shughuli fulani na hukitaji chombo kile kwa sababu hata jina linaweza kubadilika wakati wowote.

Mhe. Spika, kwa mfano kwamba sote tunajua tunao mawaziri hapa na tunajua baada ya Rais kutangaza Baraza la Mawaziri anachapisha majina pamoja na nafasi zao katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Lakini hata siku moja tukiletewa mswada haisemi hapa Waziri wa Fedha au Waziri wa Sheria na Katiba, isipokuwa inasema Waziri anayesimamia Masuala ya Katiba na Sheria kwa wakati ule na hata sheria hii ukitizama na wala hii haitaji Waziri wa Mawasiliano, isipokuwa inasema Waziri mwenye dhamana ya masuala ya usafiri baharini.

Sasa hii maana yake nini, inatoa fursa kwamba wakati wowote kadri itakavyorekebishwa basi bado Waziri yule atakayekuwa anasimamia suala lile ndiye atakayekuwa Waziri dhamana.

Kwa hivyo, na hapa nilitegemea mimi vile ilivyo tangu awali Mhe. Spika ilikuwa inatosheleza kabisa, kwamba hatukatai ushirikiano lakini chombo chochote kitakachokuwepo kule basi kitakuwa kwa jina lolote kitakuwa kinafanya ushirikiano na chombo ambacho kipo Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi sijaona mantiki ya marekebisho haya yaliyoletwa kwenye kifungu cha 6(3) (a) cha sheria mama inayorekebishwa.

Vile vile niseme kwamba mbali ya kukikosoa kuitaja *SUMATRA*, kama lengo la kifungu hichi kwamba tunadhani kitasaidia kupunguza tatizo au maafa yaliyotutokezea kwa kuweka mashirikiano, kwa sababu usafiri upo sana baina ya Zanzibar na Tanganyika, mimi sioni kama litasaidia sana na kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika.

Kwa kweli nakubali kwamba yapo matatizo ya msingi ndani ya Zanzibar ambayo yamefafanuliwa kwa kina katika ripoti zile za uchunguzi. Lakini kuna suala moja tusijaribu kulifumbia macho Mhe. Spika, takribani ajali zote mbili zilizotokezea vyombo vyake vimeanzia safari kutoka Dar-es-Salaam, yaani huko kwenye *SUMATRA*, vyombo vyote viwili *MV. Spice Islander* na *MV. Skagit*.

Kutokana na hali hiyo, ajali zilizotokezea safari zake zilianzia Dar-es-Salaam ambapo kule *ZMA* haina mamlaka kule na mwenye mamlaka kule ni *SUMATRA*. Mhe. Spika, hiyo maana yake nini, kama kuna uzembe katika usimamizi basi hata kule upo chini ya *SUMATRA* na hiyo *border line* labda itakuwa ni muarubaini ndio matatizo yetu.

Mhe. Spika, nasema mbali ya kupinga kutaja *SUMATRA*, lakini hata kama dhana yenyewe ni kwa kuleta ushirikianao ndio tutapunguza ajali, basi ingethibitika kwamba vile vyombo vilivyokuwa vimeanza safari kule visingepata ajali.

Lakini zaidi tunajua kwamba imethibitika kama kuongezeka watu pamoja na kuwa wamejazwa kwa wingi hapa Zanzibar, lakini walishaongezwa tangu Dar-es-Salaam na imethibitishwa hiyo kwenye ripoti. Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi ndio nasema kifungu hichi kidogo kinanipa mashaka.

Nikiondoka hapo naomba nije kwenye kifungu cha 6 cha mswada na hichi kinarekebisha kifungu cha 7 cha sheria mama. Mhe. Spika, hapa nataka nipongeze hasa pale kwenye (ii) inaposema Mhe. Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 6(a) (ii) kinaeleza hivi:-

> "Kubadilisha maneno "Zanzibar Tanzania" yanayojitokeza baada ya maneno "Usajili wa" na badala yake kuweka neno "Zanzibar". Marekebisho hayo yatatumika kila sehemu ambapo maneno "Zanzibar Tanzania" yamejitokeza kwenye Sheria hii".

Mhe. Spika, napongeza kwa sababu ni lazima tuwe na uwiano pamoja na usawa katika matumizi ya maneno hasa jina la nchi. Kwa mfano, Katiba ya Zanzibar inatambua jina la nchi hii ni Zanzibar na wala sio Tanzania Zanzibar. Kwa hivyo kwa kubadilisha na kuweka neno Zanzibar kila pahala naiunga mkono. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nimeona baadhi ya maeneo na natambua hilo kabisa kwamba hasa inapokuja katika masuala ya usajili imetamka Tanzania Zanzibar nayo inatambulikana, kwa sababu mpaka hivi sasa bado katika ulimwengu wa kimataifa inayotambulikana ni Jamhuri ya Muungano.

Kwa maana hiyo, kama tumeamua kuwa na usajili wa Bara mbali na Zanzibar mbali kuna kuandika Tanzania Zanzibar kwa masuala ya usajili hilo halina pingamizi mpaka hapo Zanzibar itakaporejeshewa mamlaka yake kamili ndani na nje, yaani kitaifa na kimataifa basi sina shaka na hapo tutakuja kufanya marekebisho mengine Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba niende katika kifungu cha 9, hichi kimeongeza kifungu kipya cha 10 a. Hichi vile vile nakipongeza kwa sababu ni katika yale maeneo ambayo niliyosema yanaongeza udhibiti kwa wanaoendesha biashara hii ya usafiri baharini. Kwa hivyo yale maeneo ambayo yalitajwa katika ripoti zile za uchunguzi yanafanyiwa kazi. Kwa mfano kifungu hichi kinasema:

Kifungu cha "10a (1) Hakuna mtu au taasisi itakayoingia katika shughuli zozote zinazohusiana na usafiri wa baharini bila ya leseni au kibali kinachotolewa katika namna itakayoelezwa na Mamlaka.

Kifungu cha “10a (2) Mtu yeyote atakayevunja masharti ya kifungu kidogo cha (i) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atahukumiwa kwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua dola elfu tano”

Mhe. Spika, napongeza ingawa linanipa wasi wasi, nilikuwa najiuliza ina maana kabla ya kuingizwa kifungu hichi kipya palikuwepo watu walikuwa wakifanya shughuli hizi bila ya ruhusa ya Mamlaka inayohusika kwa Zanzibar. Na kama ilikuwa hivyo inaonekana kwamba kulikuwa na uzembe wa hali ya juu. Lakini nasema pamoja na hayo madamu kwamba kumeonekana kuna upungufu huo na kinaingizwa kifungu hichi, nakipongeza.
Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba niingie kifungu cha 12 cha Mswada. Hichi watu wengi wamekizungumzia kinazungumzia sheria mama kurekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 17a mara baada ya kifungu cha 17 kama ifuatavyo. Na kifungu cha 17 a (1) kinasomeka hivi:

Kifungu “17a (1) Hakuna meli ambayo itazidi umri wa miaka 15 tokea tarehe ya kutumika kwake, itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa ajili ya kuchukua abiria na mizigo Zanzibar.”

Mhe. Spika, wamesema Waheshimiwa Wawakilishi wengi hapa kwamba ile Tume ya Uchunguzi ambayo sote tumeipa sifa kubwa kwa kazi iliyofanya ya ajali za meli, ilipendekeza kwamba umri wa meli za kusajiliwa uanzie na miaka 20 na nimemsikia Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Muyuni hapa akisema kwamba hata Ikulu ndiyo ilivyokuwa imependekezwa. Mimi siko Ikulu Mhe. Spika, sina uhakika na hilo. Lakini nasema kama ni hivyo ni suala la kuzingatia.

Ninachotaka kukisema mimi zaidi ni kuunga mkono ile hoja kusema kwamba pamoja na kutambua kwamba uchakavu chombo unaweza kwa kiasi kikubwa kuchangia ajali, lakini pekee hauwezi kuwa ndio kinga au kizuizi cha ajali Mhe. Spika.

Wenzangu wametaja hapa meli ambayo inafanya kazi katika Ziwa Tanganyika MV ILEMBA Wanasema kwamba ina umri wa miaka 100. Katika miaka ya karibuni pia niliwahi kushuhudia Malikia wa Uingereza akiuza meli yake ambayo ilikuwa ina umri mkubwa sana na mpaka leo inafanya kazi.

Mhe. Spika, sasa tunachojifunza ni nini? Na Mhe. Hamza Hassan Juma nilitaka nimlipe hapa, yupo, maana kazungumza sana habari ya chuma. Wanasema ukuukuu wa chuma si upya wa boriti. Ninachotaka kusema kwamba upya peke yake si sifa, anaweza akawemo kijana shababi humu kama Mhe. Issa Haji Ussi, lakini pengine juu ya upya wake akashindwa na ukuukuu wa Mhe. Spika, katika baadhi ya shughuli kutokana na ukakamavu wake. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimekutolea mfano kwa sababu nakuamini katika chombo hichi katika mtu mkuukuu lakini mzima kwa shughuli moja ni Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninachotaka kusema kwamba upya peke yake isiwe ndio kigezo cha kupima au cha kuona kwamba ndio tunaweza kukinga ajali kama zilizotokezea. Suala la msingi ambalo linakosekana katika nchi yetu na nchi nyingi za Afrika ni kutokuwa na utamaduni wa kutunza *maintenance*. Na hili linatokana na dharau na kutokujali, wala hili halihusu meli tu aaah! hata Beit-el-ajab, hatuna utamaduni huo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tutakuja wakati wake ukifika *In shaa Allah* Kikao cha Machi tutakuja kujadili ripoti za Kamati hapa. Tunatadharisha mambo humu humu ndani, mimi shahidi. Mwaka juzi katika Bajeti 2011 nilizungumzia uchakavu wa majengo yetu ya kihistoria, nikamwambia muhusika, limepuuzwa. Mwaka jana katika bajet nikatahadharisha tena nikasema mimi nimetembelea nikaleta na swali kwa Mhe. Waziri muhusika, nikataja na mradi ambao kuwa ulikuwa na fedha za majengo yake kwamba yashughulikiwe. Wakasema kwamba tuko mbioni, mbioni hatimaye Beit-el-ajab limeporomoka.

Sasa tunachosema tatizo Mhe. Spika, sio suala la upya tu ni suala la kuwa na utamaduni wa kuangalia mali zetu, vyombo vyetu na kuvitunza na kuvifanyia matengenezo kila baada ya muda. Hata mwili wa binaadamu Mhe. Spika, kama haufanyiwi *checking* kila wakati na ukafanyiwa *service*, maradhi yatakuwa kila wakati yanakusumbua, hata umri wako utaupunguza.

Mhe. Spika, nilichoona katika kifungu hichi cha 12 kinachoongeza kifungu cha 17a kinajaribu kutwambia kwamba dawa ya ajali ni kupunguza umri huu wa vyombo vya kusajiliwa. Wengine wamesema hapa kwamba labda hili lina lengo la kumpendelea mtu fulani. Mimi siamini hiyo Mhe. Spika. Lakini kusema kweli kadiri tukipata vyombo vipya, mradi tu ni bora na vina nguvu zinazotakikana ya kuweza kufanya kazi zinazokusudiwa basi tutafurahi. Lakini ninachosema kwamba isiwe kuweka hivi ndio itakuwa tumekinga ajali. Unaweza ukawa na chombo kipya kabisa kimetoka kutegenezwa lakini kikawa chini ya viwango. Kama hatusimamii na kama hatuna utamaduni wa kufanya kazi zetu itakuwa tunarudi pale pale Mhe. Spika. Ninachosema tusiwapotoshe wananchi kwa kuwaambia kwamba tatizo ni uchakavu tu wa vyombo. Inaweza ikawa ni sababu au kwamba ufumbuzi wa hili ni kuwa na vyombo vipya. Utakuwa na chombo kipya lakini kama kipo chini ya kiwango na vyombo vyetu vya usimamizi havifanyi kazi ya kusimamia viwango, tutajikuta tunarudi pale pale.

Ninachosema mimi hili naomba tuliangalie tena Waheshimiwa wengi wamependekeza kama ile miaka 20 imependekezwa na Tume za Uchunguzi ambazo zilifanya kazi kitaalamu, zikafanya utafiti mwahala mwingi au hiyo aliyoisema Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama imetoka Ikulu. Tuelezwe hapa kwanini tusi *adapt* hilo pendekezo letu.

Lakini ukiondoa kifungu hicho cha kwanza Mhe. Spika, vifungu vidogo vya kifungu hichi kinachopendekezwa (2), (3), (4), mimi hivi navipongeza sana, kwa sababu hivi vinakataza mambo ambayo yamekuwa chanzo cha ajali hizi. Kwa mfano watu kuchukua meli au boti za kusafirisha watu katika maeneo machache na vikajakuongezewa ghorofa ndiyo haya ambayo yanajaribu kukingwa na kifungu hichi. Hivi vifungu vidogo cha (2), (3), (4), mimi hivi navipongeza na sina matatizo navyo na hata hichi cha (1) sina matatizo nacho, nataka marekebisho ambayo yatakidhi yale yaliyopendekezwa.

Mhe. Spika, nikoondoka hapo naomba kidogo nigusie kifungu cha 13 ambacho pia kimegusiwa sana na Waheshimiwa Wawakilishi. Kifungu cha 13 hichi naomba nikizungumze kabisa kwa sababu kinawiyana na kifungu cha 17. Hichi cha 13 kinasema:

Kifungu cha 13 “Sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo:

Kifungu cha 18A Waziri anaweza kutunga Kanuni zitakazoeleza ukomo wa umri wa meli zisizokuwa za abiria kusajiliwa au kupewa leseni Zanzibar."

Kama ilivyosemwa hapa hii anaweza Mhe. Spika, inatupa mashaka sisi. Hiyo hiyo unaikuta katika kifungu cha 17 kinachorekebisha kifungu cha 43 ambacho pia kimeongezwa kifungu kidogo cha (4) kinasema:

Kifungu cha 17(4) "Waziri anaweza kutunga kanuni za usajili sambamba na mambo mengine yanayohusiana na hayo."

Mhe. Spika, ukitumia neno anaweza ambapo kwa kiingereza ni *may* badala ya neno *shall* kwamba atatunga kanuni, umempa uhuru. Zinatumika katika sheria lakini katika yale mambo ambayo hatuna uhakika. Je, kuna ulazima wa kuwa na kanuni hizo au hakukuwa na kanuni unamuachia madaraka waziri akatafakari. Lakini haya mambo mawili yaliyotajwa hapa hivyo hatujajiridhisha ikawa ni chombo cha kutunga sheria na serikali iliyoleta Mswada huu kwamba kuna haja ya lazima ya kuwa na kanuni hizi. Kwa sababu hapa panazungumzwa nini?

Panazungumziwa kanuni zitakazoeleza ukomo wa umri wa meli zilizokuwa za abiria kusajiliwa au kupewa leseni Zanzibar. Hivyo hatuhitaji kuwa na kanuni? Tunahitaji. Sasa kama tunahitaji kwa nini tuseme anaweza. Anaweza inampa uhuru kwa jambo ambalo pengine yeye mwenyewe apime kwa uwezo wake na bila shaka ni binaadamu mwenye tafakuri, lakini kwamba unahitaji au huhitaji. Lakini haya yanahitajika katika usafiri wa baharini.

Kama hichi cha 17 vile vile Kanuni za Usajili. Sasa kanuni za usajili tunashaka kama zinahitajika au hazihitajiki mpaka kutumike neno kwamba anaweza. Nilikuwa nasema Mhe. Spika, hili la kanuni nadhani liwekwe vizuri ili hii sheria isomeke vizuri hapa kwamba *'Waziri atatunga Kanuni'* kwa maneno yote mawili ambayo yametajwa hapa.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo pia kwa uchache tu niseme naipongeza serikali kwa hili. Kifungu cha 27 na kifungu cha 28, hivi zimeongezwa vifungu vipya au vijifungu vidogo vidogo vyengine vipya katika vifungu vilivyokuwepo ambavyo vinaongezea masharti kwa wanaoendesha biashara hii ya usafiri wa baharini kuwapa mafunzo kwa mfano mabaharia na kuongeza huduma muhimu katika vyombo vyao ili kuweza kutunza maisha ya watu. Kwa hivyo hivi mimi Mhe. Spika, naviongeza.

Kabla sijatoka katika Mswada Mhe. Spika, naomba Waziri akija anisaidie. Mswada huu umeishia kwa kifungu cha 29 na nimeuangalia wa kiingereza vile vile umeishia katika kifungu hicho hicho. Hivi vijitabu tuliyogaiwa asubuhi hapa hii kuanzia ukurasa wa 6 imeongezea vifungu vyengine ambavyo katika Mswada humu hatuvioni. Lazima nikiri wakati Waziri anawasilisha Mswada sikuwemo ndani ya ukumbi, lakini nimefuata kungalia hii Miswada ambayo ninayo, kama alivigusia katika hotuba yake sijui. Lakini kama hajavigusia vitanipa shida wakati wa kazi tutakapokuja kuupitisha huu Mswada.

Mhe. Spika, kuna vifungu hapa 122a kimeongezwa, kuna kifungu kimeandikwa 12(2) mimi nimekitafuta humu katika hii Sheria Mama naona kama hakipo na hakikubaliani, sasa sijui kama kimekusudiwa 122 hapa badala ya 12 labda pengine ni makosa ya uchapaji. Kuna vifungu vyengine pia vimeongezwa huku mwisho, katika Mswada wa Kiingereza na wa Kiswahili

tumeona katika hilo. Niliwauliza wenzangu hapa wakanambia tumeambiwa kwamba hii ndio imejaribu kuingiza yale marekebisho yanayofanywa katika vifungu vinavyohusika visomeke vizuri. Lakini hivi ni vipya havimo katika huu Mswada. Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija anisaidie kuhusu hivi.

Ingawa nasema tena vikiwa vimekubalika na chini ya uongozi wako Mhe. Spika, tukiingia katika kamati mimi nitaviunga mkono kwa sababu ni katika jumla ya vifungu ambavyo vinaongeza nguvu na masharti kwa wanaoendesha biashara hii. Kwa mfano huu mtaji wa bilioni tatu kwamba uwekezwe.

Naomba nikisome kifungu hicho:

> "Kuongezwa kifungu kipya kidogo cha 12(2)"

Mhe. Spika, kipo ukurasa wa 6 wa karatasi hii tuliyopewa. Sasa mimi nimekiangalia 12(2) najiuliza kinaingia pale kweli, sijui au kama imekusudiwa 122, sina hakika. Lakini kimesema:

> "Mtaji uliowekezwa na Kampuni ya meli ambayo itasajiliwa kwa kuendesha shughuli za kibiashara za usafiri Zanzibar isipungue chini ya bilioni tatu"

Mhe. Spika, mimi hiki nakiunga mkono kwa sababu tumeona hapa na nashukuru hata huku mwisho imezungumziwa mambo ya kuweka bima kwa ajili ya abiria. Tumeona hapa kuna watu wanaendesha biashara, wamepata ajali watu zaidi ya 2,000 wamepoteza roho zao, wengine wameumia, wengine wamepata matatizo ya kisaikolojia, ilipokuja kulipwa fidia wamelipwa laki nne. Serikali ikasema hizi ndio zile ambazo zimechangwa na watu waliotoa ubani au kifuta machozi au maafa. Lakini wenye dhima hasa ya kuwalipa fidia ni wenye vyombo. Ni sahihi kabisa na ndio utaratibu wa dunia nzima.

Lakini sasa huyo mwenye chombo kama hana mtaji kama huo tuna uhakika gani kama yakitokezea haya maafa anaweza kuwalipa. Mimi nakipongeza lakini nasema tatizo langu ni kwamba sikukiona katika Mswada na ndio maana nimeuliza kwamba hichi kimeingia wapi.

Mhe. Spika, pia kwa muda mchache kidogo ningetoka nje ya Mswada na mimi naomba kuna mambo ya jumla niyagusie kidogo. Mengine nimeshayatumbukiza katika mchango wangu, wakati nataja vifungu mbali mbali.

Mhe. Spika, kwanza nasema tulipoikataa SUMATRA chombo tulichokipa dhamana Zanzibar ni *Zanzibar Maritime Authority (*ZMA*)* na chuma chake hiki hapa, sheria yake nzima imewekwa humu. Wamesema wenzangu hapa kwamba unaweza ukawa na mamlaka lakini kama huiwezeshi haiwezi kufanya kazi yake. Wataalamu ndio wenye uzoefu wa kazi hizi wametwambia hapa mambo mbali mbali yaliyokuwa yapo katika matatizo ya udhibiti na uendeshaji wa suala hili la usimamizi wa usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, pametajwa hapa na hili ni tatizo sugu na si kwa sheria hii tu, kwa sheria nyingi sana lakini hii ni muhimu kwa sababu inahusu maisha ya watu, kwamba mpaka hii leo sheria hii ya mwaka 2006 leo ni mwaka 2013 ni miaka 7, lakini mpaka leo sheria muhimu kama hii inayogusa maisha ya watu kwa nchi ya mazingira ya Visiwa ambapo wasafiri wake kila siku wako katika

bahari, kanuni zake hazijatungwa. Ukiwauliza ZMA wanasema kila siku wanaiambia wizara na kila mwaka wanaomba fedha hizo na wanasema fedha zenyewe ni milioni 70. Mimi sijui milioni 70 zinahitajika kwa shughuli gani, wenyewe ndio wanajua na watakuwa wameainisha katika mahitaji yao. Hivyo kwa kanuni zinazoongoza shughuli muhimu kama hizi ikiwa hazipo hii ZMA itakuwa inaongozwa na nini katika kufanya kazi zake? Haya ndio mambo ya kuyatizama.

Jengine pia wanalalamika kwamba uongozi wa Wizara ukija utakuja kutwambia hapa. Kwamba hata vile vitendea kazi vyao na mahitaji mengine hawana. Uzuri wa ZMA na sheria hii si kwamba inaratib, lakini pia inaingiza mapato kwa serikalini kwa shughuli zake. Wanachosema kwamba mahitaji yao yote ni 570 milioni ndio wanaweza wakapata vifaa vyote vya kufanyia kazi, lakini wanashindwa kupatiwa.

Tunajua uwezo wa serikali yetu, tunajua uwezo wa nchi yetu, pengine haziwezi kupatikana zote kwa pamoja lakini haya kama alivyosema Mhe. Spika, ni maisha ya watu hasa watu wa Visiwa vya Unguja na Pemba ambapo saa zote usafiri wao ni baharini. Maneno ya Mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame anasema wengine wakisafiri wakenda wanakwenda na tweka wakirudi wanarudi na tweka. Sasa katika hili hebu tutizame mahitaji yao, katika kutunga kanuni lakini pia hayo mahitaji ya vifaa milioni 70 kwa nini zinashindwa kupatikana kuiwezesha ZMA kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika jengine kwamba kuna malalamiko kwamba ZMA yenyewe katika hii *process* yote hii haikushirikishwa hata katika kufanya haya marekebisho. Lakini hata mwana sheria wao ZMA pia hakushirikishwa. Wanasema kwamba ile sheria inataka wawepo na wanasheria. Na ni kawaida vyombo kama hivyo vinatakiwa wawe na *legal counselor* wao lakini mpaka leo hawajapewa na pengine hawawezi kumuajiri kwa sababu bajeti yao kama nilivyozungumza hapa haitolewi. Mhe. Spika, nasema kwamba tuna matatizo kwamba tunaunda vyombo lakini halafu hatuviwezeshi kufanya kazi zake. Ndio tunarudi pale pale kwamba ni wazuri wa kutunga sheria lakini usimamizi na utekelezaji wa sheria unatatizo.

Mhe. Spika, mimi sijawahi kufika Zambia lakini ninavyoambiwa na waliowahi kufika Zambia, sio wale wa Kamati zako, hawa ni wengine. Zambia utaratibu wao wa kutunga sheria, wanapopeleka sheria wanakuwa pia wameshafanya *costing* ya utekelezaji wa sheria. Bunge la Zambia linapotunga sheria linajua athari ya matumizi ya fedha katika utelelezaji wa sheria, kwa hiyo wanakuwa wanajua kwamba tuna uwezo nayo au hatuna uwezo nayo. Wakijua kama hawana uwezo nayo wanasema haina haja ya kutungwa, maana itakuwa ndio ipo ipo tu na sisi kwetu hebu tutizame hilo. Vyombo hivi kama havikushirikishwa itakuwa bado hatujafanya kitu.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa naomba Waziri akija anisaidie kwamba Sheria hii Mama imeanzisha *registry* mbili, kuna usajili wa vyombo vya ndani, lakini pia kuna usajili wa Kimataifa ya Zanzibar. Ambao wenzetu ndugu zetu wa damu inawauma sana, kila siku inatafutwa kila mbinde kwamba ifutwe. Mimi nasema kama kuna matatizo ya usimamizi suala jengine, lakini huwezi kutukosesha mapato kutwambia tufunge kitu ambacho kwa Zanzibar kinatusaidia sana hasa kwa mazingira yake kama kisiwa.

Mhe. Spika, ninachotaka kukizungumzia kwamba sheria siku zote unaitunga lakini unapoanza kuitekeleza ukaona matatizo yake unafanya marekebisho. Mwaka jana hapa palizuka mkasa

mkubwa sana katika suala la usajili wa meli za mafuta za ki-Iran. Bahati mbaya kutokana na siasa za Kimataifa zilivyo zilitaka kutuingiza katika mtihani kidogo. Bila shaka kuna matatizo pengine katika usimamizi wake au pengine katika sheria, hebu Mhe. Waziri akija atwambie katika hili. Hawakuona haja katika kufanya marekebisho na kuitia nguvu katika sheria au sijui katika Kanuni au kama ni katika usimamizi atatwambia katika usimamizi katika kulifanyia kati hili ili lisije likatuathiri huko mbele kwa mazingira yetu, nilikuwa naomba Mhe. Spika.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka pia Mhe. Waziri aje anisaidie sheria hii kwa kiasi kikubwa kama nilivyosema imeongeza nguvu za masharti kwa wamiliki wa vyombo. Lakini kuna suala zima la uokozi, hili katika ripoti zile za Tume zote mbili zimazungumzwa kwa kina sana jinsi nchi yetu ilivyokuwa haijajiandaa. Mhe. Spika, hili sio katika ripoti, sisi wengine ambao tulishiriki na tulikuwepo pale pale tumeona kwamba serikali yenyewe haipo tayari kwa lolote yanapotokezea maafa. Hakuna maandalizi ya aina yoyote, hakuna *coordination*, hakuna uratib, hakuna yupi anaemjua yupi, Mawaziri wanavutana pale pale tukiona, wao na watendaji wao wanavutana, mpaka matusi ya nguoni wanajibizana pale. Yote hayo inaonenakana kwamba watu hawana maandalizi. Tuliletewa hapa sijui mikakati ya kukabiliana na maafa na mambo mengine lakini utekelezaji ukija yote ziro. Kwa makaratasi tu ndio haya Mhe. Spika, chuma hichi hapa, lakini ukija katika hali ya utekelezaji hali tunaiyona hairidhishi.

Mhe. Spika, nasema haya marekebisho yameligusia kidogo katika wamiliki na masuala ya vyombo lakini mbona hatujaiona sheria hii ikiongezewa nguvu. Kwa mfano katika masuala mazima ya Mamlaka hiyo hiyo na mamlaka mengine kuongezewa nguvu katika masuala ya uokozi, katika sheria na baadae pia katika vyombo na vitendea kazi zinavyohitajika ili kuweza kukabiliana. Hilo Mhe. Spika, ni muhimu sana kwa sababu ajali ni ajali unaweza kuwa na vyombo vipya vyote lakini bado Mwenyezi Mungu anaweza akaleta dharuba ikatokezea ajali na dharuba huwezi kuizuia wala huwezi kuitungia sheria. Sasa ikitokezea unataka kukabiliana na maafa kama hujajiandaa, tutakuwa tunarudi pale pale. Hili suala la uwokozi naomba hili nalo pia nipewe maelekezo.

Mhe. Spika la mwisho kabisa nataka nirejee kule nilipowahi kusema siku moja kama ndio maelekezo ya kufungia maelezo yangu. Nilisema mwanzo Mhe. Spika, kwamba nakubali na mimi natofautiana na wenzangu waliosema kwamba sheria hii ilikuwa haina haja ya marekebisho. Hapana, marekebisho yanayokuja mengine ni ya msingi, kuna maeneo madogo ambayo tunaweza tukarekebisha. Lakini narejea kule tulipokuwa tukijadili ripoti ya uchunguzi wa kadhia mbali mbali nilipokuwa nikitoa mchango wangu mwisho nilimnukuu yule mwandishi *Michela Wrong* aliyeandika kitabu “IT IS OUR TURN TO EAT” kuhusiana na masuala mazima ya ufisadi na rushwa katika Afrika.

Mhe. Spika, tunaweza tukafanya marekebisho hayo na tukafanya tuyapitishe wala waziri asiwe na wasi wasi. Tukatunga kanuni, tukaja tukaongeza vyuma vyengine hata zaidi ya 100 kama hivi. Lakini kama hatuna watu ambao wamesafisha nyoyo zao wakaziweza nafsi zao, wakatekeleza wajibu wao, wakawacha kutegemea kipato kisichokuwa halali yao, ili kupindisha sheria na kusimamia utekelezaji wake, basi matatizo yatakuwa hayeshi. Alisema Mhe. Wrong na nakumbuka nilimnukuu hapa akisema kwamba:

> *“What we need is not new legislation or new institution, what we need is good people”*
> Hatuhitaji sheria mpya, hatuhitaji taasisi mpya, tunahitaji watu wema.

Mhe. Spika, hilo ni tatizo kubwa sana kwamba watu wetu kiasi gani wanasimamia. Na hili tusiwatupie watendaji tu, kuanzia sisi tunaopewa dhamana ya kusimamia ikiwa wizara ikiwa Kamati, ikiwa unakatiwa chako unakauka kifua, unakuja kutetea jambo si kwa sababu unaliamini na lina maslahi ya watu lakini kwa sababu umekatiwa chochote nje huko. Au ukiwa umepewa dhamana ya Wizara ukapindisha ukaja na masharti kwa sababu unataka kum-*favour* mtu fulani kwa sababu kakupa chochote. Katika hali kama hiyo hata tukitunga sheria kiasi gani bado hatuwezi kunusuru maisha ya watu wetu.

Nilikuwa nasema hili nilitumie kulifungia kwamba pamoja na kwamba tunapongeza na tutapitisha marekebisho haya lakini turudi pale pale kwamba vipi tunasimamia dhamana ya utekelezaji wa kazi ambazo tumepewa. Na hapo ndio linapokuja swali kwamba serikali kiasi gani iko makini, kiongozi wa shughuli za serikali ambaye ndiye mratibu wa shughuli za serikali anae *coordinate* kazi wa wizara zote na idara zote ni kiasi gani afisi yake ipo makini. Tunapotoa maamuzi humu ndani ni kiasi gani tupo makini kuyatekeleza au ndio tumepokea halafu tukisha tunayatia mkobani tukisha tunarudi tena kuja kupitisha sheria nyengine. Mhe. Spika, hayo ni ya muhimu sana ili kujiridhisha kwamba kweli tumekusudia kunusuru maisha ya wananchi wetu na sisi tuingie katika dunia ambayo inaheshimu maisha ya watu wake na hata ya wageni ambao wanatembelea katika nchi yetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nataka niseme kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Mji Mkongwe nitaunga mkono Mswada kwa yale maeneo machache ikiwa nitapatiwa maelezo ambayo yatakinaisha kiu yangu. Mhe. Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe muda uliobaki sio mzuri wa kutosha na tumejipangia shughuli nyengine mara baada ya Kikao hiki. Hivi nadhani niwaombe wale ambao niliwataja mapema kwamba nitawaita, waniwie radhi shughuli hiyo tuje tuifanye kwa kadiri tutakavyokubaliana hapa.
Waheshimiwa Wajumbe tulipanga na tulikubaliana katika *briefing* kwamba leo baada ya kipindi hichi tunachomalizia tumsikilize *Professor* Shivji ambaye tukutane naye muda mfupi baada ya kukubaliana hapa na jioni kusiwe na shughuli kama hizi utaratibu wa shughuli zetu, kama hivyo ndivyo basi niombe Waziri atoe hoja ili tumudu kwenda kwa utaratibu huu kwamba jioni tusije kwa leo na kikao chetu hichi tukiakhirishe mpaka kesho saa 3:00, ili tupate wasaa wa kushiriki katika hiyo shughuli tuliyojipangia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Spika, naomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweka kanuni kando ya kurudi katika Kikao chetu wakati wa jioni na badala yake Mhe. Spika, uliakhirishe Baraza hili hadi kesho saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha kikao tunaombwa tuhudhurie katika semina fupi ya majadiliano mafupi kuhusiana na suala zima la kuhitaji maoni ya chombo hichi kama taasisi kwenye suala la mabadiliko ya Katiba. Mkutano huo tutafanyia kwenye ukumbi

wetu wa juu, mara baada ya kuondoka humu nani. Kwa hiyo Waheshimiwa Wajumbe wote mnaalikwa tushiriki katika shughuli hiyo.

Niombe radhi tu kwamba kulikuwa na mawasiliano tofauti. Barua zilitengenezwa mwanzo kwamba tungekutana kuanzia asubuhi. Lakini kwa *tightness* ya shughuli zetu tulikubaliana kwenye *briefing* kwamba asubuhi tuwe tunakuja kwenye shughuli zetu kama kawaida na baadaye mchana twende kwenye shughuli hiyo.

Basi baada ya kukubali hivyo naomba sasa niakhirishe kikao hichi hadi kesho tarehe 18/1/2013 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi*
*tarehe 18/1/2013 saa 3:00 Asubuhi)*